USAHAULIFU WA KIROHO

Sasa naamini, sasa naamini,
Mambo yote yawezekana, sasa naamini;
Sasa naamini, sasa naamini,
Mambo yote yawezekana, sasa naamini.

2 Na tuendelee kusimama kwa muda kidogo tu kwa ajili ya Neno la Bwana. Hebu na tufungue Amosi, nabii Amosi, mlango wa 3, kuanzia kifungu cha kwanza.

3 Ninataka kumshukuru Dada Juanita na Anna Jeanne na Dada Moore, kwa ajili ya pambio hiyo nzuri ya nyimbo. Ilinirudisha nyuma, wakati nilipoketi pale nikiusikiliza. Nilikuwa nikiwazia, wakati walipokuwa pamoja nasi, wakiimba kwenye ule uamsho, mimi na Ndugu Jack tulikuwa tukizungumza, hao wasichana walikuwa ni wasichana wadogo, kumi na sita tu, kitu kama hicho, msichana. Sasa, nafikiri, Dada Anna Jeanne anao watoto watano, naye Dada Juanita ana—ana. . .mama wa watoto wawili. Nasi kweli tuko karibu na yale machweo ya jua, wanawake, kuliko tulivyokuwa wakati huo, tofauti ya kama miaka kumi na sita hivi. Haitachukua muda mrefu, tutavuka ng'ambo ya pili, wakati huo mzuri sana.

4 Sasa katika Amosi mlango wa 3, hebu tusome.

> *Lisikieni neno hili alilosema BWANA juu yenu, enyi wana wa Israeli, juu ya jamaa yote niliowapandisha . . . kutoka Misri, nikisema,*
>
> *Ni ninyi tu niliowajua. . .jamaa zote zilizo duniani; kwa sababu hiyo nitawapatiliza ninyi . . .* uovu *wenu.*
>
> *Je! Watu wawili wanaweza kutembea pamoja, wasipokuwa wamepatana?*
>
> *Je! Simba atanguruma mwituni, asipokuwa na mawindo? Mwana-simba atalia pangoni mwake, ikiwa hakupata kitu?*
>
> *Je! Ndege ataanguka mtegoni juu ya nchi, mahali asipotegewa tanzi? Mtego utafyatuka juu ya nchi, bila kunasa kitu cho chote kwake?*
>
> *Je! Tarumbeta itapigwa mjini, watu wasiogope? Mji utapatikana na hali mbaya, asiyoileta BWANA?*
>
> *Hakika Bwana. . .hatafanya neno lo lote, bila* kuwafunulia *watumishi wake manabii* siri *yake.*
>
> *Simba amekwisha kunguruma, ni nani asiyeogopa? Bwana. . .amenena, ni nani awezaye neno ila kutabiri?*

Na tuinamishe vichwa vyetu.

5 Bwana Yesu, jalia hili, Neno Lako, Bwana, jalia tuwe na ushirika usiku wa leo kwenye sehemu hii. Tunaomba, Bwana, ya kwamba utatupa somo kwa ajili ya fungu hili la maneno, tutakalochukua kutoka hapa, na jalia likuletee Wewe heshima. Tubariki tunapongojea, Bwana, usiku wa leo, juu ya Neno Lako. Waponye wagonjwa na wanaoteseka. Waokoe waliopotea. Wape nguvu walio wanyonge, Bwana, wanaodhoofika, kimwili na kiroho pia. Na utupe umwagikaji mkubwa wa Uwepo Wako, kwa kuwa tunaomba katika Jina la Yesu. Amina.

6 Ningependa kuchukua kwa ajili ya somo, kutoka kwenye hili, usiku wa leo: *Usahaulifu Wa Kiroho*.

7 Msisahau, kesho, ni maombi kwa ajili ya wagonjwa kesho. Tunamtarajia Bwana kufanya mambo makubwa mno, kesho alasiri saa nane, ambapo sisi . . . wakati tutakapoanza ibada zetu. Mvulana atakuwa hapa kusambaza kadi za maombi. Na kila mtu ataombewa ambaye anataka kuombewa. Nasi tunatarajia wakati mzuri sana, kesho, katika Bwana.

8 Sasa ninyi watu mpo hapa, mkitembelea kutoka nje ya mji. Kumbukeni, yapo makanisa mazuri, ya full Gospel kote jijini. Mmekaribishwa kwenye hayo yote.

9 Nilikuwa tu nikizungumza na mmoja wa wachungaji wenzangu, huko nje, ambaye ndiyo kwanza aingie, Ndugu Jackson, hapo awali akiwa ni wa kanisa la Methodisti, huko chini mji mmoja ama miwili chini yetu.

10 Na ni wangapi walio hapa ambao wanahusika na maskani, hebu tuione mikono yenu, kila mahali. Jamani, hakika—hakika ninafurahi kuwa nanyi huku chini. Huu ndio mkutano wa karibu sana na Indiana ambao nimekuwa nao kwa muda mrefu. Ninawazia juu ya kurudi, karibuni sana, na kupiga hema na kuzihubiri hizo Baragumu saba za mwisho, Bwana akipenda.

11 Kwa hiyo, sasa, lakini kumbukeni kesho. Msisahau jambo hilo, kesho saa nane. Na, sasa, ibada yetu ifuatayo itaanza juma lijalo, huko Tampa, Florida.

12 Sasa ninataka kuzungumza juu ya: *Usahauli- . . . Usahaulifu Wa Kiroho*.

13 Sasa, maskini jamaa huyu tunayenena habari zake, Amosi, kwa muda kidogo tu, kupata msingi wetu kabla hatujaliendea somo. Hii ilikuwa ni kwenye wakati wa ufanisi mkuu huko Samaria. Israeli ilikuwa imefanikiwa. Walikuwa kweli wameufuata ulimwengu na wakafanikiwa.

14 Si sikuzote ambapo ufanisi ni ishara ya baraka za kiroho, bali wakati mwingine ni kinyume chake. Watu wanafikiri labda inakubidi kuwa na mali nyingi ya ulimwengu, na inaonyesha kwamba Mungu anakubariki. Hiyo si kweli. Wakati mwingine ni vinginevyo.

15 Lakini tunaona, yeye, hatujui mengi kumhusu maskini mtu huyu. Yeye, hatuna historia, mahali alikotoka. Tunajua yeye, kulingana na Maandiko hapa, yeye ni mchungaji, bali Mungu alikuwa amemwinua.

16 Ninaweza kuwazia kuona, kwenye siku moja yenye joto kule Samaria, mmoja wa miji mashuhuri ya kitalii duniani siku hizo. Inalingana na, tungesema, Miami, ama—ama Hollywood, Los Angeles, baadhi ya mahali kama hapo, mahali pakubwa pa watalii. Nasi tunaweza tu kuwazia tukimwona. Hakuwa kamwe ameingia kwenye mji kama huo. Lakini, alikuwa na Neno la Bwana, alikuwa akija kwenye mji huu mkubwa ambapo dhambi ilikuwa imelundikana kila upande. Wahudumu wote walikuwa wameliacha Neno la Mungu, nao hawakuwa wamempata nabii kwa miaka mingi sana.

17 Na kwa hiyo maskini jamaa huyu, alipokipanda kilima, kwa namna fulani kaskazini tu mwa Samaria, ninaweza kuwazia nikimwona, huku jua kali likiangaza chini, na masharubu yake yenye mvi juu ya uso wake, na maskini macho yake yakasinyaa, na maskini kichwa chake, chenye upara, kiling'ara, wakati akiangalia chini juu ya mji huo. Ndipo macho yake yakasinyaa. Yeye hakuwa akiangalia yale watalii wanayoona kwa kawaida, kwenda kwenye mji na kuona tamasha zake zote za kupendeza na kuvutia sana. Aliangalia na kuona jinsi mji huo ulivyoonekana, mji ambao wakati mmoja ulikuwa ni mji wa Mungu, nao ulikuwa umezama katika kilindi cha utovu wa uadilifu jinsi hiyo. Si ajabu . . .

18 Maskini jamaa huyu mdogo asiyejulikana, alikuwa ni nabii Amosi. Na sasa hatujui mengi kumhusu. Hatujui mahali anapotoka. Manabii kwa kawaida hujitokeza jukwaani, pasipo kujulikana, kisha wanaondoka vivyo hivyo. Hatujui wanakotoka, wanakoenda, hatujui habari zao za nyuma. Mungu huwainua tu. Yeye hakuwa wa kupendeza sana ukimwangalia, bali alikuwa na BWANA ASEMA HIVI. Hilo ndilo jambo muhimu ninaloliona. Bila shaka, yeye alikuja Samaria kuanza uamsho wake. Nina hakika hakuwa na ushirikiano kutoka kwa mtu yeyote. Hakuwa na kadi ya ushirika kutoka kwa dhehebu lolote. Hakuwa na utambulisho wa kuonyesha alitoka kwenye kundi lipi. Na, ila, yeye alikuwa na jambo moja, alikuwa na Neno la Bwana kwa ajili ya mji huo.

19 Nami nashangaa, kama tungaliweza kumhamisha Amosi, leo, kumleta kwenye wakati wetu, nashangaa kama angekaribishwa katika mji wetu leo hii. Nashangaa kama tungempokea, ama tungefanya tu kama walivyofanya wao. Tunaiona miji yetu ikiwa kwenye uozo ule ule. Nasi tunaona ya kwamba dhambi ni nyingi vile vile miongoni mwa watu, kama ilivyokuwa wakati ule. Nami nashangaa, kama maskini mtu huyu mdogo, asiyejulikana, ataanzaje uamsho huu? Vipi, je! ataanzia wapi? Ataenda kwenye kanisa gani, ama ni nani

atakayeshirikiana naye? Hakuwa na kitu cha kuonyesha mahali alikotoka, hakuwa na kitu hata kidogo ila BWANA ASEMA HIVI kwa mji huo.

20 Yeye aliwakuta wameoza sana na kupotoka kiadilifu, ulikuwa ni wakati mkuu. Wanawake katika mji huo walikuwa wamekuwa karibu na walivyo Marekani. Walikuwa wamepotoka. Kila kitu ambacho Mungu alikuwa ametarajia kutoka kwao, walikuwa wameenda moja kwa moja vinginevyo. Na—nasi tunaona ya kwamba palikuwa ni mahali mashuhuri ambapo walikuwa na madansi mtaani, wanawake wakivua nguo zao kizinifu, na kadhalika, kama wavuao nguo wakicheza. Hakika, huko kulikuwa kujitumbuiza hadharani siku hizo, sasa ni kila siku. Acha tu hali ya hewa iwe joto, nawe hutakuwa na haja ya kwenda kwenye maonyesho yoyote. Wote wako mtaani, mahali popote, kwa vyovyote vile. Aibu kwenu enyi wanawake, kufanya jambo kama hilo! Hivi hamjionei aibu?

21 Halafu basi—halafu basi nilimwambia mwanamke fulani hivyo hapa, si muda mrefu uliopita, naye akasema, "Mbona," akasema, "Ndugu Branham," kasema, "hivyo, hivyo—hivyo ni kama tu hao wanawake wengine."

22 Nikasema, "Lakini haitupasi kutenda kama watu wengine. Sisi ni tofauti. Sisi ni wa—watu tofauti."

23 Inanikumbusha juu ya mwanamke fulani, alisema, "Vema, Ndugu Branham," mwingine alisema, "Mimi si—si—sivai hizo kaptura." Kasema, "Navaa suruali."

24 Nikasema, "Hizo ni mbaya zaidi." A-ha! "Mungu alisema, 'Ni chukizo,' machoni Pake, 'kwa mwanamke kuvaa mavazi yampasayo mwanamume.'" Hiyo ni kweli kabisa.

Mmoja alisema, "Vema, hawatengenezi nguo zingine zozote."

"Wangali wanatengeneza cherahani na wana vitambaa."

25 Hakuna udhuru. Ni kile tu kilicho moyoni. Hicho ndicho kinachoonekana nje. Kina—kinajitambulisha chenyewe.

26 Na sasa tunaona, katika mji huu, uliharibika kimaadili. Wahubiri waliogopa kusema jambo lolote kulihusu. Na, walikuwa na maskini, maskini jamaa huyu mdogo akikwea kilimani, alikuwa akija kuwaambia BWANA ASEMA HIVI, "Kitakaseni kitu hiki, la sivyo mtaenda utumwani." Naye aliishi kuona siku za kutimizwa kwa unabii wake. Alitabiri katika siku za Jeroboamu wa Pili, ambaye alikuwa tu ni mtu aliyetengwa na jamii, kwa vyovyote vile; a—aliyapendelea mataifa mengine. Na—na maskini huyu Amosi alitabiri akawaambia, akasema, "Mungu yeye yule mnayedai kumtumikia, Yeye atawaangamiza." Naye aliwaangamiza.

27 Na kama sauti yake ingekuwa hapa usiku wa leo, katika ninii…katika Birmingham, ingedai jambo lile lile

kwa makanisa. "Mungu yeye yule mnayedai mmemtumikia, atawaangamiza siku moja." Siizungumzii wasikilizaji hawa hapa. Kanda hizi zinaenda kote ulimwenguni. Sasa, kumbukeni, hiyo ni kweli.

28 Ndipo akaona, wakati alipoingia mjini, ya kwamba yeye . . . upuuzi huu wote, nashangaa jinsi hapana budi alijisikia kuangalia na kuona uozo huo wa watu wa Mungu, ambao alitumwa kwao.

29 Sijui kama tungempokea sasa? Kama angaliingia, je! tunge—tungeshirikiana naye? Tunge—tungejitolea kwake kabisa? Tungemsikiliza? Tungetubu kama alitwambia ya kwamba inatupasa kulirudia Neno la Bwana na kufanya vile Mungu alisema tufanye?

30 Nashangaa vile dada zetu wangefanya kuhusu nywele zao zilizokatwa? Je! wangeziacha nywele zao zikue tena, kama Amosi angalikuja? Yeye angehubiri jambo hilo, nami ninawaambia hivyo, kwa sababu hilo ni Neno la Bwana.

31 Si—sijui kama ha—halmashauri zetu ambazo zinawatoa mashemasi, waliooa mara tatu ama nne, na—na kadhalika namna hiyo, na kujaribu kuwa mashemasi, nashangaa kama mambo haya yote. Nashangaa kile angemfanyia mwanamume ambaye angemwacha mke wake avae kaptura na kutoka nje kule mtaani, na kukata nyasi uani, huko nje uani, wakati wanaume wanapita? Nashangaa angesema nini kwa mwanamume kama huyo?

32 Hakika angelikemea kwa yote yaliyo ndani yake, kwa kuwa alikuwa na BWANA ASEMA HIVI, wala asingefanya jambo lingine lolote ila hilo. Aliwakuta siku hiyo wakiwa na ugonjwa mbaya, usahaulifu wa kiroho, na huo hasa ndio tulio nao leo hii.

33 Sasa, yeye alijuaje kile kitakachotukia? Amosi angejuaje? Kwanza, yeye alikuwa ni nabii. Na, jambo lingine, yeye alibaini ugonjwa huo vile dalili zake zilivyokuwa, naye angejua matokeo yake.

34 Kama daktari akiangalia madhara na kuona ya kwamba madhara hayo yamekwisha kuingia, yeye anajua hakuna kitu kilichosalia ila mauti. Hivyo tu, isipokuwa Mungu afanye jambo fulani kuhusu jambo hilo.

35 Vema, wakati unapouangalia mji, na kuwaangalia watu, ukiliangalia kanisa, na kuwaangalia watu walio mbali sana na Mungu, hakuna kitu cha kubaini ila, "Dhambi! 'Na mshahara wa dhambi ni mauti.' Ni kufa." Ubaini huo huthibitisha kwamba ni kitu gani. Mnaona, wakati watu wanapomwacha Mungu wala hawatalisikiliza Neno, hawana tena hamu ya Neno, basi kuna ubaini mmoja kwake, "Nafsi itendayo dhambi, nafsi hiyo itakufa.' Kutokuamini kutakutenganisha na Mungu." Hiyo ni kweli kabisa.

36 Hiyo, alijua ugonjwa huo, matokeo yake, wakati alipouona ugonjwa huo wa—wa dhambi mjini.

37 Sasa, usahaulifu huu, tunaambiwa ni—ni—ni . . . unakufikisha mahali ambapo huwezi kujitambua mwenyewe. Sasa, ni jambo lisilo la kawaida. Halitendeki mara nyingi sana, lakini unasababishwa na mshtuko. Ni mtu ambaye hata hajui wao ni akina nani. Unaupata kutoka vitani, wakati mwingine, askari huupata. Wakati mwingine watu huupata. Kitu kingine kinachousababisha, ni hofu. Hofu itausababisha.

38 Hofu haina manufaa, hata kidogo. Naam, a—a—achana tu na hofu, na uikubali imani.

39 Mtu fulani alisema, "Vema, sasa, vipi kama utapigwa risasi asubuhi, hivi usingekuwa na hofu?"

Nikasema, "La, sidhani."

"Kwa nini?"

Nikasema, "Hofu isingefanya kitu ila kuifanya hali yangu kuwa mbaya zaidi."

"Vema, kuwa na imani kutakuwa na manufaa gani?"

Nikasema, "Huenda ikanikomboa." Na hiyo ni kweli, mnaona.

40 Kwa hiyo hofu haina manufaa, hata kidogo, bali imani ina manufaa yote. Amininі!

Sasa hofu wakati mwingine huusababisha.

41 Na jambo lingine linalousababisha miongoni mwa watu, ni kuingia katikati ya maoni mawili. Huko kutasababisha usahaulifu. Nako kunakufikisha mahali ambapo wewe—wewe, kwa kweli, yale umefanya, umeingia kichaa. Umerukwa na akili. Huwezi kuninii . . . Hujui u nani wewe. Huwezi kujitambua. Unaweza kutembea huku na huku, kula na kila kitu, ila, wewe, ungali huwezi kujitambua. Una elimu yako ya shule, unaweza . . . elimu ile ile uliyokuwa nayo, bali hujui imetoka wapi, hujui u nani wewe, kwamba wewe ni wa wapi. Huo ni usahaulifu, ndivyo tunavyoambiwa.

42 Tunatambulishwa na familia zetu, katika maisha haya ya kibinadamu, kwa ndoa. Na pamoja na wake zetu, tunafunga ndoa, na familia yetu inatambulishwa kwa muungano wa ndoa ye—ye—yetu. Ndipo basi, la kuwazia, vipi kama jambo hili baya sana lingekupata wala usingeweza kukumbuka ulifunga ndoa na nani, mke wako ni nani, watoto wako ni akina nani, baba na mama yako ni nani, jirani yako ni nani? Hilo lingekuwa ni jambo ba—baya sana.

43 Ndipo tunatambulishwa, tena, tunaweza kujitambulisha wenyewe katika jamii ya binadamu, kwa kuwa na akili na—na kuwa tofauti na uhai wa wanyama. Mnyama hawezi kuwaza, yeye anatumia tu sauti. Hana nafsi. Na, bali, sisi ni uhai wa

wanyama. Kinachotufanya tofauti...Sisi ni mamalia, lakini kile...Mamalia ni mnyama mwenye damu moto, nasi tuko katika maumbile ya mnyama. Lakini kile kinachotufanya tofauti, tumetambulishwa kwa kuwa na nafsi, dhamira inayotwambia yaliyo mema na mabaya.

44 Sasa kuna mahali, unapoupata usahaulifu huu, unaweza ukawa kama Nebkadreza, huyo ndiye, ambaye alijitukuza wakati mmoja, ndipo Mungu akamwacha afikirie kwamba yeye ni mnyama. Naye aliishi huko nyikani na—na kula nyasi kama maksai. Na—na niniii zake—nywele zake zikakua mwilini mwake, kama manyoya ya tai, naye akapata moyo wa mnyama ndani yake. Mnaona? Huo ulikuwa ni usahaulifu, kwa sababu alikuwa amesahau ya kwamba alikuwa ni mfalme. Alikuwa amesahau kwamba alikuwa ni mwanadamu. Naye alifikiri alikuwa ni mnyama, kwa hiyo akatenda kama mnyama, kwa sababu alisahau alikuwa ni mwanadamu.

45 Hilo ni rahisi sana, leo. Nasi tunasahau, wakati mwingine, kwamba Kanisa la Kikristo ni kitu gani. Tunatenda kama walimwengu. Hiyo inaonyesha ya kwamba tuna usahaulifu wa kiroho, kwa sababu hutendi kama Mkristo. Unatenda kama walimwengu. Unaupokea moyo wa ulimwengu, nao unasababisha jambo hili.

46 Hapa tu—tunaona ya kwamba Israeli walikuwa wamejianika, walianikwa kwa ulimwengu, nao walikuwa wameingia katika mkondo huu. Naye nabii huyu alikuwa ametumwa kuwafukua, kama angeweza, na kuwaambia. Mungu, kwa neema Yake, aliwachagua Israeli kutoka katika jamaa zote zilizo duniani. Neema ilikuwa imefanya jambo hilo. Alikuwa amewapa nchi iliyo nzuri sana. Aliwapa nyumba ambazo haikuwabidi kujenga. Mungu alifanya hivyo, aliwachagua. Aliwapa mashamba ambayo hawakununua. A—aliwapa, aliwapa chakula ambacho hawakupanda. Aliwapa visima ambavyo hawakuchimba. Aliwapa ushindi ambao hawakushinda. Aliwapa neema ambayo hawakustahili. Mungu alifanya jambo hilo kwa neema Yake kwa ajili ya watu hawa, Israeli, aliowachagua, aliowapenda.

47 Naye akasema, katika Biblia, "Alimpata kondeni, kama msichana mdogo ameketi juu ya damu yake mwenyewe, Naye akamwosha na kumsafisha, na yale aliyofanya. Lakini baada ya Mungu kumwonyesha rehema hizi zote, na akatajirika," akashikwa na usahaulifu, usahaulifu, "ndipo akasahau ambapo vitu hivi vyote vilitoka."

48 Nafikiri hiyo ndiyo picha ya Marekani, 1964. Inaugua ugonjwa ule ule. Sisi ni makanisa makubwa yenye nguvu. Sisi ni watu wakuu, wenye nguvu. Tuna idadi ya mamilioni, nasi tumesahau ambapo mambo haya yalitoka.

49 Walikuwa na ugonjwa mbaya. Baada ya Mungu kuwafadhili, na kuwatoa katika nchi zote za makafiri, na kuwafanya watu waliotengwa, akawatenga wawe Wake. Alisema, "Yeye alichukua mzabibu kutoka nchi nyingine na kuupanda katika nchi nyingine, na jinsi alivyoutengeneza kuufanya uzae tunda na kuzaa matunda, bali mzabibu huo ukasahau mahali baraka zake zilipotoka."

50 Vivyo hivyo na watu wa Mungu, katika siku hizi za mwisho, wamesahau ushuhuda wa kuwa Mkriso una maana gani. Mara nyingine tena, usahaulifu huu umewashika watu. Hawawezi kujitambua.

51 Wao, walisahau Hayo yote. Walisahau utakatifu Wake. Walisahau torati Yake. Wanawake walikuwa wakiishi kama wanawake wengine.

52 Kanisa la Mungu na watu Wake daima wamekuwa, "Watu waliotengwa, wa—watu walioitwa watoke, watu wa kipekee, taifa takatifu, ukuhani wa kifalme; wakimtolea Mungu dhabihu za kiroho, matunda ya midomo yao, wakilisifu Jina Lake." Mungu aliliita Kanisa Lake na kulitenga na ulimwengu, kwa kusudi lilo hilo. Naye akalipa amri, na Yeye, Hilo, halina budi kuwa takatifu. Yeye alisema, "Mimi ni mtakatifu, nanyi hamna budi kuwa watakatifu, na pasipo na utakatifu hamna mtu atakayemwona Bwana." Mungu alisema hivyo, Yeye Mwenyewe.

53 Naye alikuwa amewaita watu hawa wawe watu wa namna hii, bali walikuwa wamesahau hilo. Walikuwa wamesahau amri Zake, nao walikuwa wamesahau maadili yao. Wanawake huko mitaani, wanawake Waisraeli huko nje, kila mmoja wao akitarajia ku—kupata mimba kwa Roho Mtakatifu, apate kumzaa Masihi, halafu kutenda namna hiyo. Tabia zao zilikuwa ni mbaya sana.

54 Nataka kusimama hapa kwa dakika moja, kusema ni jambo lile lile miongoni mwa watu wetu, leo hii, wanaojiita Wakristo. Tabia yao, laiti mngalitambua!

55 Wakati mmoja, huko Kusini. Nilisoma hadithi moja kutoka huku chini, ambako wakati walipokuwa na watumwa. Wangewachukua watu hao na kuwauza sokoni, kama tu vile ungaliuza gari lililotumika. Na ndipo kulikuwako na mnunuzi mmoja, dalali, angekuja na kuwachukua watumwa hawa na kuwauza, kama tu vile ungeuza gari ama chochote kile.

56 Na hao watumwa walikuwa mbali na nchi ya wenyeji wao. Walitoka Afrika. Makaburu waliwateka nyara, wakawaleta huku visiwani, na kisha kuwaingiza Marekani kimagendo na kuwauza kama watumwa, kutoka huko Jamaika na kwingineko huku.

57 Sasa tunaona ya kwamba watu hao walikuwa na huzuni. Walikuwa wametekwa nyara kutoka nchini mwao. Walikuwa

wamechukuliwa na adui, nao walikuwa na huzuni. Kamwe hawatawaona waume wao tena, ama mke wao tena, baba na mama zao, watoto wao. Walikuwa ninii kabisa. . . Iliwabidi kuwacharaza, kwa mijeledi, kuwafanya wafanye kazi, kwa kuwa walikuwa ni watu wenye huzuni.

58 Basi siku moja, dalali alipitia shamba fulani, akaona kundi la watumwa huko nje wakifanya kazi. Ndipo a—akaingia na kumwuliza mwenyewe, kasema, "Una watumwa wangapi?"

Akasema, "Karibu mia moja."

Kasema, "Una yeyote ambaye ungetaka kumbadilisha kwa mwingine ama kumuuza?"

Akasema, "Naam."

Kasema, "Hebu niwakague."

59 Basi akaenda kondeni na kuwaangalia, naye akaona iliwabidi kuwacharaza kweli. Na baada ya kitambo, akamwona kijana mwanamume mmoja haikuwalazimu kumcharaza. Alikuwa kifua mbele na ameinua kidevu chake; haikuwalazimu kumcharaza. Kwa hiyo huyo dalali akasema, "Ningetaka kumnunua yule mtumwa."

Naye akasema, "Lakini hauzwi."

60 Akasema, "Vema, tofauti yake yule mtumwa ni nini?" Kasema, "Je! yule mtumwa ndiye bosi juu ya hao wengine?"

Akasema, "La, yeye ni mtumwa tu."

Akasema, "Vema, labda unamlisha tofauti."

Akasema, "La, yeye hula manchani pamoja na watumwa wengine."

61 Akasema, "Vema, ni kitu gani kinachomfanya tofauti sana na watumwa hao wengine?"

62 Akasema, "Vema, hili lilinishangaza, pia, kwa muda mrefu. Lakini siku moja nikasikia, kwamba, huko nchini mwao anakotoka, baba yake ndiye mfalme wa kabila zima. Na ingawa yeye ni mgeni, na mbali na nyumbani, hata hivyo anajua yeye ni mwana wa mfalme, naye—naye anajiadhibisha kama mwana wa mfalme."

63 Nikawazia, "Lakini, jambo hilo, kama Mnegro anayetoka Afrika, na anajua ya kwamba baba yake alikuwa wa kabila fulani na ni mfalme juu ya kabila moja, inapaswa kumfanya nini Mkristo aliyezaliwa mara ya pili, mwanamume ama mwanamke, kwamba Baba yetu ni Mfalme wa Mbinguni Utukufuni!" Tunapaswa kujiadhibisha kama wanaume na wanawake Wakristo. Tunapaswa kuenenda jinsi hiyo, kuvaa jinsi hiyo, kunena jinsi hiyo, kuishi jinsi hiyo. Ingawa sisi ni wageni, hata hivyo tu wana wa Mfalme. Amina.

64 Tabia yetu, upotovu wetu katika siku tunazoishi sasa! Israeli walikuwa wameshika njia ile ile na pia walikuwa ni

waovu. Walikuwa wamezisahau amri za Mungu, "Usizini, wala usimtamani mke wa jirani yako," na kadhalika. Walikuwa wamesahau amri hizo. Ha—ha—hawakuzitaka tena. Nao—nao walitaka ku—kuwa kama walimwengu wengine, kama vile tu kanisa limekuwa siku hizi.

65 Wakati mmoja, Israeli, walipoanza, walitaka kuwa na mfalme juu yao. Samweli akawaambia, nabii waliyetumiwa, akasema, "Sasa nimewahi kuwaambia jambo lolote katika Jina la Bwana ila lililotimia?"

Wakasema, "La, hujawahi."

66 "Je! niliwahi kuwaomba chakula changu na pesa, pesa zenu, pia, nipate riziki?"

67 "La, hujafanya hivyo. Kamwe hukutwambia lolote, Samweli, ila lililotimia. Wala kamwe hujatuomba fedha zetu, upate riziki yako. Lakini, hata hivyo, tunataka mfalme, haidhuru."

68 Mungu akamwambia Samweli, "Acha wampate. Hawakukukataa wewe, walinikataa Mimi."

69 Israeli walikuwa wameingia kwenye hali hiyo hiyo sasa. Hawakutaka manabii wa Mungu tena. Hawakuwahitaji. Na kama mmoja angekuja, na kuwaletea Neno, na kujaribu kuwarudisha kwenye Neno, wangekataa Hilo. Daima wanafanya jambo hilo, katika njia hiyo ya upotovu.

70 Wakati ulimwengu na kanisa vinapoungana pamoja, basi hawataki kitu chochote cha kiroho. Hawataki BWANA ASEMA HIVI. Wanataka kile wanachotaka. Wanautaka ulimwengu, na kusema wao ni Mkristo; na kuishi ulimwenguni, na kuishi pamoja na ulimwengu, na kuishi kama walimwengu, na bado wadumishe maungamo yao ya kuwa Mkristo. Mnajua, jambo ni kwamba, ni usahaulifu wa kiroho. Hivyo ndivyo ulivyo hasa. Hawajijui. Wamesahau yale wanayopaswa kufanya.

71 Kama mmoja angekuja leo hii, namna hiyo, lingekataliwa vivyo hivyo. Walikuwa na hali mbaya sana ya huo, na ndivyo walivyo siku hizi. Wasingeweza kujitambulisha na mambo ya kimbinguni, tena, kwa sababu hawakuyataka. Neno, Injili, hawakuitaka. Ugonjwa wa dhambi ulikuwa umewatesa, nao waliupenda.

72 Dhambi ni tamu kwa moyo usioongoka. Inaonekana ni nzuri kwa moyo usioongoka, bali ni njia ya mauti. Hakuna kilichosalia ila mauti. "Mshahara wa dhambi ni mauti," nawe huna budi kuvuna mishahara hiyo. Umepanda upepo, na sasa unavuna tufani.

73 Ishara za kiroho na mahubiri ya mjumbe aliyechaguliwa kutoka kwa Mungu, hayakuwasisimua tena. Wanawake wangewacheka machoni pao, na kusema, "Hainibidi kwenda kusikia upuuzi kama huo." Kama jambo hilo halijajirudia

tena! Ni kitu gani? Usahaulifu wa kiroho, ndivyo ilivyo hasa. Wamesahau ya kwamba Mungu na Neno Lake ni kitu kile kile, wala hawezi kulibadilisha.

74 Kama nabii alijitokeza jukwaani katika siku hizo na kutoa ishara ya kiroho, sauti ya kiroho, na kutoa sauti ya Mungu nyuma yake, wangelicheka tu Hilo na kulifanyia mzaha.

75 Mnajua ule msemo wa kale, "Wapumbavu hutembea kwa viatu vya njumu mahali ambapo malaika wanaogopa kukanyaga." Hivyo ndivyo usahaulifu huu wa kiroho hufanya. Huwafanya watu wafikie mahali ambapo hawana hisi ndani yao. Hawataki chochote ambacho ni cha kiroho.

76 Hebu chukua mkutano halisi wa kiroho, ambapo Roho Mtakatifu anawaponya wagonjwa na kuyatambua mawazo yaliyo moyoni, na uuweke miongoni mwa makanisa yote, mkutano mkubwa tu kwenye uwanja huu wa michezo, na uangalie jambo litakalotukia. Katika dakika chache, kila mtu angekuwa akiamka na kutoka nje. Hawana uhusiano wowote nalo. Hawataki uhusiano wowote nalo. Watasikiliza hotuba fulani ya kiakili.

77 Lakini inapofikia kwenye Nguvu za Yesu Kristo, na kufufuka Kwake, na Roho Mtakatifu, hawataki uhusiano wowote nazo, kwa kuwa zinawahukumu. Zinawapasha moto kwa jambo wanalopaswa kujua. Hakuna kurudiwa, hakika, ni ya kupendeza kwa muda. Lakini, hiyo, kama utajitolea kwake, zi—zitaleta matunda ya toba. Kwa hiyo tunaona, wakati usahaulifu huu wa kiroho unapowashika watu, basi wako—wako katika hali mbaya. Sasa tunaona jambo lilo hilo sasa. Sasa ninataka kuninii . . .

78 Huna budi kutambulishwa. Mahali fulani, inakubidi kuonyesha. Maisha yako yanaonyesha, usiku wa leo, mahali unapotambulishwa. Unatambulishwa ama ndani ya Kristo au nje ya Kristo. Huko katikati. Hakuna kitu kama mlevi asiye mlevi. Hakuna kitu kama ndege mweusi mweupe. Ama umeokoka au hujaokoka. Wewe ni mtakatifu au ni mwenye dhambi, mojawapo, na msimamo wako wa kiroho kulihusu Neno la Mungu unakutambulisha mahali unaposimama hasa. Kweli!

79 Neno la Mungu, lililohakikishwa, lilithibitisha ya kwamba ubatizo wa Roho Mtakatifu ni kama tu ulivyokuwa kwenye Siku ya Pentekoste ama wakati mwingine wowote. Naye Yesu Kristo ni yeye yule jana, leo, na hata milele. Na msimamo wako kwa Hilo unatambulisha kama wewe una usahaulifu wa kiroho, ama huna. Hiyo ni kweli. Haidhuru kama wewe ni shemasi, ama hata kama wewe ni mhubiri, haileti . . . Naam, wanaipata, pia. Kwa hiyo tunaona, unaenea upesi na unaathiri kitu hicho chote. Sasa tunaona.

80 Sasa, kuwa Mwamerika. Kuwa Mwamerika, sina budi kutambulishwa na taifa langu. Sasa sikilizeni kwa makini. Kuwa Mwamerika, wakati ninapozaliwa hapa katika nchi hii, ninafanyika raia, nami ninatambulishwa na taifa hili. Yote liliyo, ndiyo niliyo mimi. Yote ambayo limekuwa, ndiyo nami niliyo. Kwa kuwa ninatambulishwa kama Mmarekani, basi sina budi kuchukua aibu yake yote, utukufu wake wote. Chochote lilicho, ndicho nilicho, kwa sababu nimetambulishwa nalo. Amina. Ninawatakeni mlipate. Nimetambulishwa kama raia wa Marekani, basi yote liliyokuwa, ndiyo niliyo mimi. Yote liliyo, ndiyo niliyo. Sina budi kuwa ni sehemu yake. Sina budi . . . endapo mimi ni raia wa Marekani, mimi ni sehemu ya Marekani. Na yote liliyo, nami pia.

81 Hainipasi kusahau jambo hili kamwe. Kama ninataka kubaki raia wa kweli wa Marekani, sina budi kukumbuka ya kwamba mimi ni kile taifa langu lilicho, kwa maana ninatambulishwa na taifa langu. Kulisahau, ama—ama . . . Kulipigania, ama kufa kwa ajili yake, ama kutetea yote linayotetea, sina budi kulitetea. Kile taifa langu lilicho, ndicho nilicho mimi. Kile linachotetea, ninakitetea. Kuwa Mmarekani mwaminifu, nitakuwa tayari kulifia, kulipigania, kulitetea, kufanya lolote lililopo. Mimi ni sehemu yake. Huwezi kulichokoza pasipo kunichokoza mimi. Unaposema jambo fulani dhidi yake, unalisema dhidi yangu, kwa kuwa mimi ni Mmarekani. Kulisema dhidi yako, kama Mmarekani, na yale wanayosema dhidi ya taifa hili, wanayasema dhidi yako, kwa kuwa wewe ni sehemu yake. Msisahau jambo hilo kamwe; mnapolisahau, basi mna usahaulifu, hakika kabisa.

82 Pia, kumbuka, wewe si raia wa Marekani tena wakati huwezi kuwa sehemu yake. Huna budi kuwa. Kile Mmarekani alicho, huna budi kuwa pia. Sina budi kulishiriki. Hili ni taifa langu, sina budi kushirikiana nalo. Kile lilicho, ndicho nilicho. Mnaona, kile lilichokuwa, ndicho nilicho. Haidhuru lilikuwa nini, mimi ningali kile lilichokuwa.

83 Kuwa Mmarekani, nilishukia Plymouth Rock, pamoja nalo, pamoja na wale wazee waanzilishi. Ilinibidi; mimi ni sehemu yake. Nilipanda farasi na Paul Revere, kulionya juu ya hatari zake. Endapo mimi ni raia halisi wa Marekani, nilishukia Plymouth Rock. Nilipanda farasi pamoja na Paul Revere, kulionya juu ya hatari yake. Mnajua ninalomaanisha sasa?

84 Nilivuka Delaware uliojaa barafu, pamoja na George Washington, pamoja na askari wake miguu mitupu. Nilikuwa kule, kwa kuwa nimetambulishwa na taifa hili. Alichofanya kule kilikuwa ni sehemu yangu; ninachofanya sasa ni sehemu yake. Nilitambulishwa pamoja na Washington, huko Delaware.

85 Nilisimama pamoja na Stonewall Jackson, wakati mambo yalipomwendea mrama sana, nao wakauliza, “Unawezaje

kusimama kama ukuta wa mawe, wakati hamna matumaini?" Maskini jamaa huyo mwenye macho ya bluu na mwenye soni akapiga mavumbi kwa viatu vyake, akasema, "Kamwe sinywi kikombe cha maji kabla ya kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa ajili yake." Sina budi kusimama kama ukuta wa mawe pamoja naye. Nilisimama pale pamoja na Stonewall Jackson. Kuwa Mmarekani, ninatambulishwa pamoja naye na msimamo wake. Kuuvuka Delaware! Kupiga vita!

86 Niliipandisha bendera. Nilikuwa pamoja nao wakati walipoiinua ile bendera huko Guam. Baada ya maelfu ya askari wa Marekani kuyatoa maisha yao, na wakati lile kundi dogo lilipokimbia kule na kuirusha hiyo bendera juu, nilitambulishwa katika kuinuliwa kwa bendera hiyo; kila mmoja wetu alitambulishwa. Raia wote wa Marekani walitambulishwa pamoja na hiyo bendera iliyoning'inia juu ya Guam. Niliposikia ya kwamba walikuwa wameipandisha bendera hiyo huko juu, machozi yalitiririka mashavuni mwangu. Huyo alikuwa ni mimi. Huyo alikuwa ni wewe. Hiyo ilimaanisha sisi sote, wakati tulipotambulishwa pale pamoja na hiyo.

87 Yote liliyo, ndiyo niliyo. Utukufu wake wote ni utukufu wangu. Aibu yake yote ni aibu yangu. Kama limefanya mambo ya aibu, basi itanibidi kulikazia. . .kuistahimili shutuma yake. Likipokea utukufu, ninapokea utukufu pamoja nalo, kwa kuwa nimetambulishwa pamoja nalo. Sasa, kutambulishwa, Mmarekani hana budi kuistahimili aibu yote ya Marekani, utukufu wote wa Marekani, yote lililopata kuwa. Yote liliyo, ama kile litakachokuwa, umetambulishwa pamoja nalo.

88 Sasa, kuwa Mkristo wa kweli, inakupasa kuwa vile vile. Hatutaki kusahau jambo hilo. Yote aliyokuwa, nimetambulishwa pamoja Naye. Nimetambulishwa pamoja Naye.

89 Angalia, Naye yumo ndani yangu, nami ndani Yake. Angalia, basi, kila Mkristo aliye Mkristo—Mkristo halisi, alikuwa pamoja Naye, "Hapo nyota za asubuhi zilipoimba pamoja na wana wa Mungu wakapiga makelele ya furaha, kabla hapajakuwapo na misingi ya nchi." Tulitambulishwa katika milki isiyopatikana na mauti pamoja na Mungu, miaka milioni kumi kabla ya ulimwengu kuumbwa. Nilikuwa kule nyuma pamoja Naye. Kama nina Uzima wa Milele, nilikuwa kule pamoja Naye. Nilitambulishwa pamoja Naye, "Hapo nyota za asubuhi zilipoimba pamoja na wana wa Mungu wakapiga makelele kwa furaha."

90 Nilikuwa pamoja Naye hapo alipomwita Ibrahimu kwenye umri wa—wa miaka sabini na mitano, na mkewe akiwa na sitini na mitano, na akamwambia watapata mtoto. Nilikuwa pamoja naye wakati alipochukua msimamo wake juu ya BWANA ASEMA HIVI, "nitampata mtoto huyo." Nilisimama pamoja

naye. Kila Mkristo mwingine alisimama pamoja naye. Nilikuwa pamoja naye wakati majaribu yake yalipokuja. Nilikuwa pamoja naye wakati alipopanda juu ya mlima, kutoa Isaka dhabihu. Nilikuwa pamoja naye wakati yule kondoo dume alipotokea.

91 Nilikuwa pamoja na Yusufu wakati alipokataliwa na ndugu zake, kwa sababu alikuwa ni wa kiroho na hao wengine walikuwa ni wa kimwili. Nilikuwa pamoja naye wakati alipoijua aibu iliyombidi kustahimili kutoka kwa ndugu zake. Kile alichokuwa, ndicho nilicho mimi. Kile nilicho mimi, ndicho alichokuwa. "Kwa maana sisi sote ni mmoja katika Kristo Yesu." Nilikuwa pamoja na Yusufu pangoni mwake, kaburini. Nilikuwa pamoja naye wakati alipoenda kwenye mkono wa kuume wa Farao. Ilikubidi kutambulishwa pamoja naye.

92 Nilikuwa pamoja na Yakobo usiku ule aliposhindana mwereka usiku kucha na Malaika. Nilishindana mwereka, mimi mwenyewe. Ninajua aliyopitia. Kwa hiyo nilishindana mwereka pamoja na Yakobo wakati ule ule alioshindana, kwa kuwa mimi ni ndugu yake.

93 Nilikuwa pamoja na Musa wakati aliposhuka kwenda Misri. Nilikuwa pamoja na Musa kwenye kichaka kilichowaka moto. Iwapo wewe ni Mkristo, umetambulishwa na wahusika hao wa Biblia. Usisahau hilo! Nilikuwa pamoja na Musa wakati watu wote walipomgeuka. Nilikuwa pamoja na Musa hapo alipoivuka Bahari ya Shamu. Hapo alipouinua mkono wake na kusonga mbele, nayo bahari ya Shamu ikafunguka, nilitambulishwa katika Kristo papo hapo, nami nilikuwa pamoja na Musa katika wakati huo.

94 Chochote Wakristo wamekuwa, chochote waaminio wamekuwa, kila mwaminio sasa ametambulishwa na mtu yuyo huyo. Chochote kile, huna budi kutambulishwa. Usisahau hilo. Ukilisahau, una usahaulifu wa kiroho; umesahau u nani wewe.

95 Sasa kutambulishwa pamoja naye, pamoja na Musa, wakati alipoivuka ile bahari.

96 Nilikuwa pamoja na Eliya katika siku za Ahabu, wakati ilipowabidi kufanya chaguo ni nani watakayemtumikia, Mungu ama Balaamu. Tulikuwa pamoja naye juu ya Mlima Karmeli, wakati ilipomlazimu kufanya chaguo hili, kwa kuwa tumetambulishwa katika Mwili wa Mungu yeye yule ambaye yeye alitambulishwa ndani Yake. Kwa hiyo ikiwa tumetambulishwa katika Mwili huo, basi hatuna budi kukumbuka tulikuwa pale pamoja naye. Hiyo ni kweli.

97 Sasa, nilikuwa pamoja na Daudi, wakati alipokataliwa na ndugu zake mwenyewe. Nilikuwa pamoja na Daudi; wewe ulikuwa pamoja naye, pia, kama wewe ni Mkristo. Inakubidi kutambulishwa katika kukataliwa kwake.

98 Nilikuwa pamoja na wale wana wa Kiebrania, katika tanuru iliyowaka moto, wakati ule—ule moto usingeweza kuwachoma kwa sababu ya Uwepo wa yule Mtu wa nne.

99 Nilikuwa pamoja na Danieli, katika tundu la simba. Nilitambulishwa mle ndani, wakati Malaika wa Bwana alipomtambulisha mle ndani.

100 Hakika kabisa nilikuwa pamoja na Yeye pale Kalvari. Sina budi kutambulishwa pamoja na Yeye pale Kalvari. Sina budi kuwa pale kufikia mahali, ambapo, ambapo si kutambulishwa tu pamoja Naye pale Kalvari, nilikufa pamoja Naye pale Kalvari. Kila Mkristo hana budi kufa pamoja Naye pale Kalvari. Usipokufa pamoja Naye pale Kalvari, huwezi kuwa Wake kamwe. Nilikuwa pale wakati alipokufa. Nilikufa pamoja Naye. Halafu nilikuwa pamoja Naye hapo alipofufuka katika wafu. Nilifufuka kwenye ile asubuhi ya Pasaka pamoja Naye, katika ule ufufuo. Lolote alilofanya, nilikuwa pale pale pamoja Naye; kila mwaminio alikuwa vile vile.

101 Na sasa nimeketi pamoja Naye katika ulimwengu wa Roho katika Kristo Yesu, huku nguvu zote za kuzimu zimeshindwa, kupitia Yeye. Kila Mkristo mwaminio alikuwa ameketi vivyo hivyo, maana huna budi kutambulishwa.

102 Sasa ninajikuta, katika siku hizi za mwisho, pamoja na Wakristo wengi waaminio, nimetambulishwa katika huduma Yake. "Ni yeye yule jana, leo, na hata milele." Ninajikuta, katika siku hii, nimetambulishwa katika huduma Yake. Je! unajikuta hivyo, ukiiamini, kutembea pamoja nayo? Angalia, kazi alizofanya Yeye, alisema mwaminio angefanya jambo lile lile. "Kazi nizifanyazo Mimi ninyi nanyi mtazifanya." Basi unaweza kutambulishwa pamoja Naye? Basi shutuma inapokuja kwenye Neno, unaweza kuvumilia shutuma kama vile alivyofanya, unaona, kutambulishwa pamoja Naye? Nilitambulishwa pamoja Naye.

103 Nilikuwa pamoja Naye kwenye Siku ya Pentekoste. Nilikuwa pamoja na wanafunzi huko juu, nimetambulishwa pamoja nao katika ubatizo wa Roho Mtakatifu.

104 Nashangaa kama kanisa halijashikwa na usahaulifu sana hata hawaninii, baadhi yao, hata hawaamini kuna kitu kama Roho Mtakatifu. Mnaona mahali kanisa limefikia? Ugonjwa mbaya sana wa usahaulifu! Mnaona, wamesahau ya kwamba huyo alikuwa ni Yesu Kristo huko nyuma. Wamesahau kile Yesu Kristo alichokuwa. Wamesahau. Walidhani alikuwa ni m—mtunga sheria tu, ama nabii, ama m—mtu mwema. Walisahau ya kwamba alikuwa ni Mungu. Walisahau kwamba ni yeye yule jana, leo, na hata milele. Nalo kanisa lina ugonjwa mbaya wa usahaulifu wa kiroho. Wamesahau mambo haya yote. Hawayafahamu tena.

105 Hatuna budi kuwa pamoja na wale mitume kwenye Pentekoste, tutambulishwe pamoja nao. Nilitambulishwa pamoja na mahubiri ya Petro kwenye Siku ya Pentekoste, katika Matendo mlango wa pili. Nilisikia aliyosema. Ninaamini aliyosema. Nilitii aliyosema. Sasa nimetambulishwa katika jambo lile lile.

106 Usishikwe na usahaulifu wa kiroho. Maana, utaninii, utajitambulisha na kitu kingine. Dumu moja kwa moja na hilo Neno!

107 Tulikuwa pamoja na Kanisa wakati lilipoagizwa na Yesu Kristo, katika Matendo, Mlango wa 16. "Enendeni ulimwenguni kote, mkaihubiri Injili kwa kila kiumbe." Ninataka kutambulishwa pale, "Ulimwenguni kote, kwa kila kiumbe." "Ishara hizi zitafuatana na hao waaminio," naweza kutambulishwa katika jambo hilo.

108 Vema, sasa, je! umetambulishwa na hilo, ama umeshikwa na usahaulifu wa kiroho, kwamba unakuta huamini ishara hizo zinawafuata waaminio? Mnaona, kama huamini hilo, basi una usahaulifu wa kiroho, unaona, umesahau ya kwamba Mungu aliahidi jambo hilo. Yeye alisema, "Ishara hizi zitafuatana na hao waaminio." Usisahau hilo. Huwezi kusahau jambo hilo na uwe Mkristo. Huna budi kutambulishwa pamoja nalo.

109 Huna budi kutambulishwa na Yohana Mtakatifu mlango wa 14, kifungu cha 12. "Yeye aaminiye pamoja na Mimi, kazi nizifanyazo Mimi yeye naye atazifanya." Usisahau hilo. Ukilisahau, basi una usahaulifu wa kiroho. Umesahau wewe ni nani. Umesahau ushuhuda wako unachomaanisha.

110 Vipi kuhusu, Yeye alisema, "Mkidumu ndani Yangu, na Neno Langu ndani yenu, mnaweza kuomba mtakalo nanyi mtapewa"? Je! umetambulishwa hapo, kuamini ya kwamba hiyo ni Kweli? Marko 11, wakati Yeye aliposema, "Ukiuambia mlima huu, 'ng'oka,' wala usitie shaka moyoni mwako, bali uamini kwamba ulichosema kitatimia, kitakuwa chako." Je! waweza kutambulishwa hapo, kuamini ya kwamba hiyo ni Kweli? Kama sivyo, basi unashikwa na usahaulifu wa kiroho.

111 Na—nawe unasahau, unapoteza urari wako wa Ukristo. Hujui unakosimama. Unasema, "Mimi ni Mmethodisti. Mimi ni Mbaptisti. Hilo ndilo ninalojua kulihusu. Mimi ni Mptentekoste. Mimi ni *hili, lile*, ama *linginelo*." Angalia! Hiyo inaweza kumaanisha ya kwamba dalili ya huo ugonjwa inaonekana kwako, ya kwamba umeambukizwa usahaulifu wa kiroho.

112 Unasema, "Vema, Ndugu Branham, ni—ninaamini jambo *hili*, na ni—ni vigumu. . . " Sasa ngoja kidogo tu. Kama Mungu aliahidi kufanya mambo haya, na kusema yangekuwa katika siku za mwisho, na kanuni zako za imani zitakuzuia usiyapate, hiyo ni ishara nzuri ninaweza kuona dalili ya ugonjwa juu yako.

Ni usahaulifu wa kiroho. Umesahau kujitambulisha pamoja na Neno.

113 Unasema, "Siamini ya kwamba wagonjwa huponywa." Una usahaulifu wa kiroho.

114 Unasema, "Siamini katika ubatizo wa Roho Mtakatifu." Usahaulifu wa kiroho!

115 Unasema, "Si—siamini ya kwamba Mungu aliahidi kufanya mambo haya katika siku za mwisho." Basi umesikiliza kanuni ya imani, ama fundisho fulani, badala ya Biblia. Una usahaulifu wa kiroho. Hujui umesimama wapi basi. Unakiri, "Mkristo," na kulikana Neno. Inakurudisha moja kwa moja kwenye usahaulifu wa kiroho tena, unaona, hujui unakosimama. Una usahaulifu wa kiroho. Huwezi kujitambulisha na Maandiko.

116 Inakubidi kuwa pamoja na mitume. Inakubidi kuwa pamoja na Maandiko yote, pamoja na Kanisa wakati limeagizwa. Lakini, sasa, wakati Kanisa lilipoagizwa, "Enendeni ulimwenguni kote mkaihubiri Injili; ishara hizi zitafuatana na hao waaminio," hilo lilikuwa ndilo agizo lake. Sasa wao wameninii . . . Hilo lilikuwa ndilo agizo.

117 Lakini wameshikwa na ugonjwa mbaya wa huu usahaulifu wa kiroho, kama tu Hawa alivyopata kwenye . . . alivyokuwa nao, huko bustanini, siku moja. Sasa yeye ni kama Israeli, akiugua ugonjwa uu huu, mzio kutoka kwenye mlo wa seminari ambao utakupa usahaulifu wa kiroho. Ukila mlo wa seminari, utapata mzio, halafu basi, muda si muda wajua, utapata usahaulifu mbaya sana. Huamini chochote Biblia isemacho.

118 Hiyo ndiyo shida ya kanisa siku hizi. Hiyo ndiyo shida hatuwezi kupata uamsho siku hizi. Hiyo ndiyo shida ya watu siku hizi. Wameleweshwa juu ya makaa ya kila kitu, na kila itikadi ingaliweza kuanguliwa, hata hawajui kweli wala uongo. Kweli kabisa. Haliwezi kumkumbuka Bwana wake. Haliwezi kulikumbuka Neno Lake. Haliwezi kuikumbuka ile ahadi.

119 Hiyo ndiyo ilikuwa shida ya Israeli, wakati Yesu alipojitokeza jukwaani. Wasingeweza kukumbuka, ya kwamba, "Bikira atachukua mimba." Wasingeweza kukumbuka ya kwamba Musa alisema, "Bwana Mungu wenu atawaondokeshea Nabii mithili yangu." Walikuwa na usahaulifu wa kiroho.

120 Huo ndio kanisa lililo nao hasa siku hizi. Yeye alisema, "Itakuwa katika siku za mwisho," ya kwamba mambo haya yatatukia, ambayo tunayaona yakitukia, nalo kanisa limeketi kitako limekufa kama saa sita. Ni kitu gani? Usahaulifu wa kiroho. Tunajiita Pentekoste, wala hatuwezi kutambua, wala hatuwezi kujitambulisha na Neno wakati limehubiriwa katika nguvu za kufufuka kwa Kristo; Naye akiwa hapa miongoni mwetu, akilitimiza, na kufanya vile hasa Yeye alisema lingefanya. Basi, angalieni, mfumo wetu wa kimadhehebu

umetuingiza katika usahaulifu wa kiroho. Tunaugua. Hatujui tumesimama wapi. Mmoja anahamisha makaratasi yake kutoka kanisa *hili* hadi kwa *lingine*, na kanisa *hili*, na itikadi *hii* na itikadi *ile*. Mnaona?

121 Tunachohitaji, tena, ni Amosi mwingine kujitokeza jukwaani, akiwa na BWANA ASEMA HIVI. Tungempokea? Ni karibu kama walivyofanya. Hawakumpokea kamwe. Wasingempokea siku hizi. Ingekuwa ni vigumu, kuingiza kichwa Chake mahali fulani, apate kuhubiri. Sasa, hiyo ni kweli kabisa, kwa sababu kanisa linaugua ugonjwa huu wa usahaulifu wa kiroho.

122 Sasa, kwa nini? Mungu aliahidi katika siku hizi za mwisho, "Wakati Mwana wa Adamu atakapofunuliwa," kulingana na Luka, mlango wa 17, "kwenye ile ishara iliyokuwa ikitendeka Sodoma, ingetukia tena." Nao watu wanaiona ikifanywa, na baadhi yao hata hawaiamini. Wanafikiri ni telepathia. Wanafikiri ni roho wa ibilisi. Ni kitu gani? Wanaugua ugonjwa wa usahaulifu wa kiroho. Hiyo ni kweli kabisa. Hawawezi kumfahamu Bwana. "Yesu Kristo ni yeye yule jana, leo, na hata milele." Kile alichokuwa wakati huo, ndicho alicho sasa.

123 Lakini, kile kimetukia, hatuwezi tu kujitambulisha tena na Neno. Kwa nini? Hilo, halijui kama ni chama ama ni kanisa. Halitaki kuitwa chama, wala haliwezi kuitwa kanisa; maana, kuitwa kanisa, kungelitambulisha na Kristo. Hilo linalipa usahaulifu wa kiroho. Wala halitaki kuitwa chama. Kwa hiyo si kanisa la Kipentekoste, kanisa la Methodisti, kanisa la Baptisti; ni chama cha Kipentekoste, chama cha Methodisti, na chama cha Baptisti, maana haliwezi kutambulishwa na Neno. Na wakati Neno linapodhihirishwa, wangali hawaliamini. Ni ugonjwa, usahaulifu wa kiroho. Hawawezi kujitambulisha wenyewe; hawajui wanakosimama. Hiyo ni kweli.

124 Ni kama tu kuzalisha kitu fulani kwa kuchanganya mbegu. Kama ambavyo nimesema mara nyingi, "Daima niliwazia moja ya vitu vipumbavu sana nilivyopata kuona kilikuwa ni nyumbu." Mnaona, yeye ni chotara. Mnaona, mama yake alikuwa ni farasi, baba yake ni punda, na wala hata hajui anakotoka. Na muda si muda wajua, utaninii, u—unaweza kumzalisha na upate punda, na halafu . . . ama upate nyumbu, bali nyumbu huyo hawezi kujizaa tena. Unaona, hajizalishi. Huwezi kumfundisha kitu. Yeye ni kichwa-ngumu. Kamwe hutaweza kusema kitu . . . Unaweza kuyatega hayo masikio makubwa na marefu. Naye atangojea mpaka siku iliyo ndefu sana ya maisha yake, kabla tu hajafa, akupige teke. Hivyo tu. Daima anaotea jambo fulani tu akushambulie, akiweza.

125 Na hilo linanikumbusha juu ya watu wengi wanaoitwa Wakristo machotara. Wamelichanganyishia kanisa mbegu hata

wamepata ugonjwa wa usahaulifu wa kiroho. Hawawezi kuzaa kitu kingine tena.

126 Wanazungumza juu ya mahindi chotara. Mahindi chotara si kitu. Ndicho kitu kibaya sana unachoweza kuweka kinywani mwako, kitu chochote chotara. Hiyo ndiyo sababu inakubidi kuchukua mimea hii ya tuta, na vitu vya kichotara, na kuinyunyizia na kuitibu na kuibembeleza. Kwa nini? Kwa sababu hawawezi kuwazuia wadudu wasiishambulie.

127 Lakini ukoo safi, ulio halisi, haikubidi kuunyunyizia viondoa wadudu. Una Nguvu ndani yake, kuwazuia wadudu wasiushambulie. Hicho ndicho kinachohitajika kuwazuia wadudu wa kutokuamini wasimshambulie mtu aliyejazwa na Roho halisi.

128 Hebu chukua maskini nyumbu, nawe uanze kumzungumzia, useme, "Aisee, jamani, ninakutaka ufanye *hili, lile*."

129 Ataketi hapo, "Hoo! Hoo! Hoo!" Hayo masikio makubwa yakiinuka na kushuka. Nimewaona wanaojiita Wakristo we—wengi, karibu namna hiyo.

130 Unasema, "Yesu Kristo ni yeye yule jana, na hata milele. Ishara hizi zitafuatana na hao waaminio."

131 "A-ha? Ninaamini siku za miujiza zimepita. A-ha? A-ha? A-ha?" Mnaona, yeye hajui anayoamini. Hajui chochote. Hajui anakotoka; hajui anakoenda. Ana usahaulifu wa farasi. Hajui anakotoka, wala hawezi kwenda mbele zaidi.

132 Bali ninapenda uzao bora na halisi. Loo, yeye ni mpole. Unaweza kuzungumza naye. Yeye anajua baba yake alikuwa ni nani, mama yake alikuwa ni nani, babu na nyanya yake walikuwa ni nani. Ana makaratasi ya ukoo safi kuonyesha alikotoka.

133 Nami nampenda Mkristo wa ukoo safi, ambaye anaweza kurejea huko nyuma kabisa kwenye Neno la Mungu, kwenye siku ya Pentekoste, na kujitambulisha wenyewe kule pamoja na watakatifu, ambapo Nguvu za Roho Mtakatifu ziliwashukia. Huyo ni Mkristo wa ukoo safi. Anajua anakotoka. Hajitambulishi na Methodisti, Baptisti, wala chochote kile. Yeye anajitambulisha katika Neno la Mungu. Anajua mahali anaposimama hasa. Damu ya kifalme ya Baba yake inatiririka ndani yake; Damu ya Yesu Kristo. Anajua kile inachofanya! Anaamini kila Neno. Mungu anatenda kazi kupitia kwake na anathibitisha hilo kwa ishara alizoahidi zitafuata. Hana usahaulifu wa kiroho. Yeye ni ukoo safi. Ninapenda hilo.

134 Lakini kanisa siku hizi lina ugonjwa mbaya wa usahaulifu wa kiroho. Halijui linasimama wapi. Lilisahau yote kulihusu, likasahau mambo haya yote yanayolifanya Kanisa.

135 Ni kitu gani kilichotutajirisha jinsi tulivyo? Limefikia mahali pa Laodikia tena, kurudi kwenye mahali pale pa utajiri

kama vile Israeli ilivyokuwa. Wakati ilipokuwa maskini na ilibidi kumtumainia Mungu kwa kila kitu ingaliweza kufanya, kila kitu ilichopata, ilimtumainia Mungu; ndipo Mungu alikuwa pamoja nayo, nayo ilikuwa ni ya kiroho, na ikaendelea. Bali ilipotajirika, hivi ndivyo ilivyotendeka: miji yao ilijengwa, na wanawake wao wakawa watovu wa uadilifu, wanaume wao wakaruhusu jambo hilo, wahubiri wao wakaachilia mambo, na wakawakanusha manabii. Na hiyo ndiyo aina ya hali waliyoingia. Kilichoisababisha hiyo, kilikuwa ni kusahau mahali hizo baraka zilipotoka.

136 Nanyi Wamethodisti, nanyi Wabaptisti, nanyi Wapresbiteri! Ninyi Wamethodisti mnaweza kumkumbuka John Wesley. Ninyi Wabaptisti! Naye John Smith alililia hali ya watu hata ikambidi mke wake kumwongoza mezani, macho yake yalikuwa yamevimba hata yakafungika, kutokana na kulia na kuomba usiku kucha. Kuna nini?

137 John Wesley alisema ya kwamba moja ya mambo makuu . . . Ninaamini ilikuwa ni mmoja wa baba waanzilishi wa Methodisti aliyesema, "Aibu ya binti za kanisa la Methodisti, walikuwa wameanza kuwa wa kilimwengu sana, walikuwa wakivaa pete kwenye kidole chao." Angesemaje sasa, huku wamevaa kaptura?

138 Ni jambo gani lililotukia? Usahaulifu wa kiroho. Ndivyo ilivyo hasa, mmesahau mlikotoka. Mnayo mambo haya yote kwa ajili ya fadhili za Mungu, wema uliwafanyia.

139 Mnafikiri hili ni jambo la kigeni? Linaambatana kabisa na Roho wa Yesu Kristo, unabii. Katika Ufunuo, mlango wa 3, ilisema, "Kwa kuwa unasema, 'Mimi ni tajiri, sina haja ya kitu,' wala hujui kwamba wewe ni maskini, kipofu, mnyonge, mwenye mashaka, uchi, wala hujui." Mnaona, hujui! Ni kitu gani? Usahaulifu wa kiroho. Hawajui.

140 Makanisa yana pe—pesa sasa. Hakuna kanisa, angalau, nchini, la kimadhehebu, lisilo na thamani ya mamilioni mara mamilioni ya dola. Wanajenga mamilioni na mamilioni ya dola katika mijengo na kadhalika, huku wakihubiri Kuja kwa Bwana kumekaribia. "'Tajiri,' na likasema, 'sina haja ya kitu.'" Wahubiri wenye elimu kuliko wote waliopata kuwa nao, wanaojua theolojia sana kuliko walivyopata kujua. Nao wana mijengo mikubwa kuliko yote, sehemu nzuri sana zilizochaguliwa mjini. Wana njia ya kupata chochote wanachotaka kufanya. Halafu basi walifanya nini? Wakashikwa na usahaulifu wa kiroho na kusahau Mungu ndiye aliyewafanyia hayo, kama tu Israeli.

141 Nayo Biblia ilitabiri, Yesu Kristo alimtuma malaika Wake kwa Yohana na kusema, wakati huu wa mwisho wa kanisa ungeshikwa na usahaulifu huu wa kiroho. Walikuwa ni "wanyonge," kumbukeni. Wanafikiri wao ni wakubwa. Wanafikiri wana kitu fulani. Ila Yeye alisema walikuwa "wenye

mashaka, wanyonge, maskini, vipofu, uchi, wala hawakujua." Wala hakuna njia ya kuwaambia.

142 Sasa, kama mwanamume angalikuwa hapa nje mtaani, ameaibika, ama mwanamke, uchi, mtaani, kipofu, hiyo ingekuwa ni hali ya kusikitisha kuwa katika hali hiyo. Lakini basi kama walikuwa na akili timamu, walijua wao ni nani, kwamba walikuwa ni wanadamu, nao wanapaswa kuvaa nguo; vema, ukitoka uende huko nje; wao—wao ni wanadamu, wanapaswa kutambulishwa na jamii ya binadamu; nao wako huko nje, "wanyonge, wenye mashaka, vipofu, na uchi." Nawe umwendee, ukisema, "Ndugu, uko uchi."

143 "Sasa, hapa! Mimi ni Daktari *Nanii*! Wewe shika lako. Nakwambia, mimi ni wa *Ninii hii*! *Huna* shughuli, wewe mtakatifu anayejifingirisha, kuniambia chochote!" [Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.]

144 Ukiwaambia, "Ni kosa kwa mwanamume kufanya jambo hili, na kwa watu kufanya mambo wanayofanya."

145 Nao watakufahamisha ya kwamba mhubiri wao ana mawazo mapana. Mnaona? Ni kitu gani? Ni, wamesahau amri za Bwana Yesu. Basi acha Yeye ashuke na kufanya ishara na maajabu aliyosema angefanya, hawataki kuamini. Ni usahaulifu wa kiroho. Mnaona, wamesahau! Nao ni uchi, wala hawajui, hawatambui.

146 Wanawazia, "Kwa sababu tu mimi ni mfuasi wa kanisa, hilo tu ndilo linalohitajika." Loo, ndugu, hilo halina maana yoyote kwa Mungu kuliko kuwa Mmasoni ama chochote kile, chama kingine chochote. Kuwa mfuasi wa kanisa, hilo halina maana yoyote kwa Mungu.

147 Hamna budi kuwa wana na binti za Mungu. Hamna budi kuzaliwa na Mungu, Naye Mungu ni Neno. Ninapofanyika sehemu ya baba yangu, ninakuwa baba yangu wote. Unapofanyika sehemu ya Mungu, unafanyika Mungu, kikamilifu. Neno Lake lote, unaliamini lote.

Usahaulifu wa kiroho!

148 Vipi kama hukujua jina lako lilikuwa jinsi lilivyokuwa? Na endapo ndivyo ulivyo, utatoka kwenye familia nzuri, ambayo natumaini ulitoka, kama unatoka kwenye familia nzuri ya watu, basi vipi kama ulisahau jina la familia hiyo, nawe ukatoka huku nje, unaishi kwa aibu? Wangesema, "Hivi jina lako si Jones," ama lolote lile. "Vema, sijui mimi nilikuwa ni nani." Mnaona? Vema, mnaona, hilo ni jambo la kuchukiza sana kuwa, ni hali ya kuchukiza sana kuingia.

149 Vema, hapo tu ndipo kanisa limefikia. Linapaswa kuwa uwakilisho wa Yesu Kristo. Bali limesahau hilo, kwa maana linaninii, limeingizia, kanuni za imani na madhehebu, kwamba

wamekubali hizo badala ya Neno. "Nao ni uchi, vipofu, wenye mashaka, wala hawajui," wala hakuna njia ya kuwaambia.

150 Huenda nisiwe Birmingham tena, lakini huu ni wakati mmoja itawalazimu kulisikia. Mnaona? Mnaona? Kweli. Ninaninii tu . . . Mimi siwajibiki kwa chochote ila kupanda Mbegu. Mungu huielekeza kwenye ardhi inakopaswa kwenda.

151 Walisahau, naam, walisahau Neno la ahadi. Walisahau. Israeli walikuwa kwenye matatizo ya namna hiyo wakati Yesu alipokuja. Walikuwa wamesahau. Waliangalia, loo, walisema waliamini kuna Masihi ajaye. Lakini Masihi alipokuja na kujitambulisha Mwenyewe kwa Neno, walikuwa na mapokeo mengi sana hata walikuwa wamelitangua Neno la Mungu.

152 Naye Yesu aliahidi, kabla tu ya wakati wa mwisho, "Kama ilivyokuwa katika Sodoma, ndivyo itakavyokuwa." Na ingetambulishwa, nao watu ni wa kimapokeo sana hata wameitangua ahadi ya Mungu, kwa mapokeo yao. Usahaulifu wa kiroho! Ni usahaulifu wa kiroho hasa. Mnaona, wameyasahau mambo haya.

153 "Loo, mimi ni mfuasi wa *hili*. Ni—nimefanya *hivi*. Nilicheza katika Roho. Nilifanya jambo *hili*." Vema, jamani, jamani, hilo halina uhusiano wowote nalo, hata kidogo.

154 Unawezaje kuwa Mkristo na kulikana Neno? Huwezi kufanya hivyo. Mungu ni Neno. Kama Neno liko ndani yako, wewe na Neno ni kitu kimoja. Yote liliyo Neno, ndiyo uliyo wewe. Amina. Kama ninaishi katika kizazi hiki, kile sehemu hii ya Neno imeahidi kwa ajili ya kizazi hiki, sina budi kuwa hicho. Endapo nitakuwa Mkristo, sina budi kutambulishwa na yote yale Biblia inayohubiri na kutetea.

155 Haleluya! Mtaniita mtakatifu anayejifingirisha, haidhuru, nami ninajisikia kubarikiwa sana sasa hivi. Naam, bwana.

156 Sina budi kutambulishwa na kila kitu ambacho Biblia inadai. Nayo hutoa madai yake, na, endapo sijashikwa na usahaulifu huu wa kiroho wa siku hizi, nitatambulishwa na ninaweza kutambulishwa Nalo. Kama nikilikana, basi nina usahaulifu wa kiroho; jambo fulani limetukia, nimekubali kanuni fulani ama fundisho, ama kanisa fulani ama kundi la watu. "Siwezi kufanya hivyo," wakati Neno bado linakuja na kujitambulisha Lenyewe.

157 Hiyo ndiyo sababu Yesu hakutambulikana. "Loo," wanasema, "vema, mtu huyu ni mtakatifu, na kuhani wetu mtakatifu, *nanii* wetu mtakatifu."

158 Naye Yesu akasema, "Ninyi ni wa baba yenu, ibilisi, na kazi zake mtazifanya."

159 Je! mnajua Kaini alitoa dhabihu nzuri, vile vile? Alikuwa ni mwaminifu, akajenga madhabahu, akapiga magoti na kuabudu, na kutoa dhabihu, na kumwomba Mungu. Na kama, Mungu,

hayo tu ndiyo Mungu anayohitaji, wewe kuwa mfuasi wa kanisa na kuwa na madhabahu, na kutoa zaka zako na kwenda kanisani, na kuishi maisha mazuri; kama hayo tu ndiyo anayohitaji, Yeye alikuwa mwonevu kumhukumu Kaini, maana yeye alifanya jambo lilo hilo. Naam, bwana. Hiyo ni kweli kabisa.

160 Lakini *dini* linamaanisha “kifuniko,” wala huwezi kufunikwa na matendo yako mema. Kuna kitu kimoja tu ambacho Mungu atakubali, na hicho ni Damu ya Yesu Kristo. Hicho ndicho kifuniko cha pekee. Nje ya Hicho, kama ukisema, “Kutii kanuni za imani,” usahaulifu wa kiroho! Hilo ndilo lililotukia.

161 Sasa angalia, wamesahau Neno lao. Wameisahau Biblia. Wameisahau ahadi. Wanajaribu kuishi katika mng’ao wa kile Methodisti ilichokuwa, kile Baptisti ilichokuwa, kile mtu mwingine alichokuwa. Hii hapa ahadi ya siku hii, Naye Mungu akiinena kupitia Neno Lake, na kuihakikisha tena na kuthibitisha kwamba ndivyo ilivyo, na wangali hawaiamini. Usahaulifu wa kiroho! Hiyo ni kweli kabisa. Wenye usahaulifu mtupu, mtupu, kabisa hawaiamini hata kidogo.

162 Askari wa Kifaransa. Nilisimuliwa hadithi ndogo; kabla hatujafunga. Sikujua ilikuwa imechelewa hivyo, nami nina karibu kurasa kumi hapa za muhtasari zilizosalia; nitaziendea wakati mwingine. Angalieni, askari wa Kifaransa. Walichukua kundi la askari kutoka kwenye jeshi, nao walikuwa na huu usahaulifu. Unatokana na mshtuko, vitani. Nao walikuwa na ratiba, nao—nao wakatangaza kwamba watu waliowapoteza wapendwa wao wapige simu waone kama wangeweza kuwatambua wavulana hawa. Hawakuwa na matumaini, labda mmoja ama wawili, kutoka kwao, walifahamu. Basi wakawachukua hao wengine, walikuwa wakitaka kuwaweka kwenye kituo cha kudhibiti afya, ambako wangekaa siku zote za maisha yao.

163 Walikuwa wakipanda kilima, wakikokotwa na garimoshi; ndipo wakasimama kwenye stesheni moja, wakawaachilia wavulana hao watoke nje na kuinyosha miguu yao. Nao walinzi wakasimama kilimani, kuwalinda, maana wakiwa na usahaulifu, mbona, i—iliwabidi kuwalinda.

164 Kwa hiyo wakamwangalia jamaa mmoja mdogo pale, alitoka na akaanza kuangalia huku na huku kwenye tangi hilo la maji, akaangalia kote kilimani. Akaupangusa uso wake, na kuchunguza vizuri. Kisha akaangalia tena, naye akaliona tangi hilo la maji. Akaangalia kote kwenye stesheni hiyo, kisha akaanza kutembea. Badala ya huyo mlinzi kumsimamisha, akamfuata.

165 Akapanda kilimani, akashuka kwenye njia ndogo ya miguu, akageuka mkono wa kuume kisha akapanda kilima kingine

kidogo, ndipo akafika kwenye nyumba ndogo ya magogo. Akaangalia. Huyu hapa mzee na fimbo mkononi mwake, akitokea barazani, akaja akamkumbatia. Kasema, "Mwanangu, nilijua utarudi. Waliniambia ulikuwa umekufa, bali nilijua ungerudi." Ndipo mvulana huyo akajirudia. Usahaulifu wake ukamwacha. Angeweza kujitambua. Alijua huyo alikuwa ni baba yake.

166 Loo, ewe askari wa Msalaba, ambaye ameshtuliwa na mafunzo mengi, mishtuko mingi ya dhehebu na kanuni za imani, na mambo ya ulimwengu, kwa nini usiondoke kwa dakika chache uende ukaichunguze Biblia? Huenda ukatangatanga, na huenda ukajikuta umetambulishwa hapa katika Neno, kama mwaminio, moja ya siku hizi. Huenda usimjue. Huenda ukajirudia, kama mwana mpotevu alivyofanya, na ujirudie. Huenda ukapata utambulisho wako katika Maneno ya Mungu.

167 Mtu fulani alisema, hivi majuzi, sio muda mrefu uliopita, kasema, "Lakini, Ndugu Branham, hebu tuangalie sisi Wapentekoste, jinsi tulivyo na makanisa mazuri. Mbona, sisi, tuna wahudumu waliofunzwa."

168 Sikilizeni, mwanamume anapomwoa mke, yeye hategemei urembo wake. La. Anategemea uaminifu wa nadhiri yake, neno lake. Hategemei urembo wake. Anategemea uaminifu wake.

169 Na hivyo ndivyo ilivyo unapoolewa na Mungu, hutegemei kanisa kubwa zuri unaloweza kujenga, bali katika ahadi iliyotolewa na Yesu Kristo, kwamba, "Mimi ni yeye yule jana, leo, na hata milele." Unaamini hilo? [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.]

Na tuinamishe kichwa chetu kwa dakika moja.

170 Sijui, usiku wa leo, humu jengoni ambamo watu wameketi, ambamo mna wanaume na wanawake walio wa Milele, watu wanaoelekea Milele, nawe unajua kwamba siku moja ama nyingine huna budi kukutana na Mungu. Nami sijui kama ulikuwa na chembe ndogo ya huo usahaulifu, nawe ungeninii . . . Umetambulishwa katika kitu kibaya, nawe unge—ungetaka kwenda huku na huku, usiku wa leo, na kuona kama huwezi kutambulishwa katika Kristo Yesu? Waweza kuinua mkono wako, useme, "Niombee, Ndugu Branham, ni—ninataka kutambulikana kama Mkristo halisi, mwaminio halisi." Mungu akubariki. Mungu akubariki. Ubarikiwe! Loo, naam, kila mahali. Bwana Mungu awabariki.

171 Mtu fulani huko juu kwenye roshani, useme, "Ndugu, kweli ninaamini hiyo ni Kweli. Ninaamini, kama Wakristo, sisi si Wakristo kama walivyokuwa miaka kadhaa iliyopita."

172 Vipi kuhusu ninyi Wapentekoste, wakati mama na baba zenu walikuwa wakisimama hapa nje mtaani, na kupiga tari ya kale. Na mama yenu, jinsi ilivyombidi kuninii . . . alichoka sana, na

kuwashughulikia sana ninyi watoto wadogo. Wakati mwingine iliwabidi kwenda bila nguo, na kila kitu kingine, bali baba na mama walikuwa waaminifu kwa Huduma, kumwinua Kristo.

173 Angalieni yale ninyi Wapentekoste mliyofanya. Miaka hamsini iliyopita, mlitoka kwenye dhehebu. Hilo ndilo linalowafanya Wapentekoste, mlijitenga na asiyeamini. "Na kama nguruwe kwenye kugaagaa kwake, na mbwa kwenye matapiko yake," mmerudi moja kwa moja na kufanya jambo lile lile, mkasababisha machafuko yale yale mliyotoka kwake. Kuna shida gani? Usahaulifu wa kiroho ulitokea miongoni mwa watu. Mna kanuni zenu za imani na makaratasi yenu ya kimadhehebu sasa, nanyi mko kule kule pamoja na hao wengine, mnataka kuwa pamoja na hao wengine. Mliwaruhusu wanawake wenu kukata nywele zao, kujipaka rangi. Ninyi, mnawaruhusu kufanya mambo haya yote, mnaruhusu upuuzi huu wote ma— makanisani. Ni kitu gani? Usahaulifu wa kiroho.

174 Halafu, muda si muda mwajua, Mungu anapoanza kuwatembelea watu, basi kunatokea nini? Hamwezi kulipokea. Mnaona, mmekuwa wagonjwa sana kwa usahaulifu huo, mnaona, jambo pekee mlilopata kusikia. Hivi hamdhani mnapaswa kuziondokea kanuni hizo za imani kwa dakika chache tu na kuichukua Biblia, mpate kuona kile Mkristo anachopaswa kutambulishwa nacho? "Ishara hizi zitafuatana na hao waaminio!"

175 Matendo, Petro alisema, "Tubuni, kila mmoja wenu, mkabatizwe katika Jina la Yesu Kristo kwa ondoleo la dhambi, nanyi mtapokea kipawa cha Roho Mtakatifu; kwa kuwa ahadi hii ni kwa ajili yenu, na kwa watoto wenu, na kwa hao walio mbali, wale watakaoitwa na Bwana Mungu wetu wamjie." Kama wakiwaambia Hiyo sivyo ilivyo, basi mchungaji wenu ana ugonjwa mbaya wa usahaulifu wa kiroho. Yeye hawezi kujikuta ametambulishwa na Kanisa hilo; si dhehebu; Kanisa, Mwili wa kisiri wa Kristo.

176 Sasa Roho Mtakatifu yupo hapa. Yeye yupo hapa kufanya vile hasa alivyoahidi kufanya. Sasa wakati mkiwa hapa huku mmeinamisha vichwa vyenu, endeleeni tu kuomba. Acheni Roho Mtakatifu anene, Mwenyewe. Na muone kama hii . . . Yeyote anajua hiyo, ile ahadi, jinsi ilivyo kwa ajili ya siku hii. Sasa ninyi mlio na haja, usiku wa leo, ninyi, wengi wenu mliinua mikono yenu. Kabla hamjafanya jambo hilo . . .

177 Nashangaa, wakati tukiwa hapa na kuwaombea wagonjwa kweli, sijui kama unaweza kuondokea huko kutokuamini, dhehebu hilo, kanuni hiyo ya imani inayokwambia mambo haya sivyo yalivyo, hiyo ambayo ingekwambia ni ya ibilisi. Wanapofanya hivyo, "Hawatasamehewa kamwe, katika ulimwengu huu wala ulimwengu ujao." Vipi kama Huu ndio Kweli? Wazia tu, vipi kama ni Kweli, basi wewe uko wapi?

Unaona, haikubidi kusema kwa sauti; amini tu moyoni mwako. Na kuna watu hapa wanaoamini hilo. Nimeketi papa hapa, kwa siku mbili zilizopita usiku, nikitaabika chini ya jambo fulani, ninii tu, jamani, nikazuia na kuuma ulimi wangu, nisije nikalitamka.

178 Basi kumbuka, ewe rafiki, ni kati yako na Mungu. Vipi kama si kweli, nawe unawazia hilo? Unajua linalotukia, kamwe hutasamehewa hilo. Usahaulifu wa kiroho, utaingia moja kwa moja kwenye mauti yako ya Milele, kutokuamini. "Yeye asiyeamini amehukumiwa tayari!"

179 Sasa ombea ugonjwa wako, useme, "Bwana Yesu, Wewe uliahidi. Mimi . . ."

Huenda kukawa na wageni hapa, ambao hawajapata kuwa hapa hapo kabla.

180 Yesu aliahidi, "Kama ilivyokuwa," nitachukua Andiko moja, "katika siku za Lutu," wakati Mungu alipodhihirishwa katika mwili wa nyama; nao watu, Ibrahimu, kundi lililoteuliwa, kundi lililoitwa litoke. Kisha jina la Abramu likabadilishwa likawa Ibrahimu, ndipo akaliona Neno likifanyika mwili, Nalo likayatambua mawazo yaliyokuwa katika moyo wa Sara.

181 Basi wakati Uzao wa Kifalme wa Ibrahimu ulipokuja, hivyo ndivyo alivyofanya, nao wakamwita "ibilisi."

182 Akasema, "Sasa Roho Mtakatifu atakapokuja, atafanya jambo lile lile." Kasema, "Sasa kuna msamaha mnaponiita hivyo, lakini, mtakaponena dhidi ya Roho Mtakatifu, hamna msamaha."

183 Sasa hebu Yeye, katika Nguvu Zake, na apitie kwenye hadhara hii ya watu, popote ulipo, pamoja na utambuzi Wake wa kiroho akionyesha ya kwamba Yeye ni Neno. Kusudi kama kuna yeyote hapa anayeugua usahaulifu, kwamba hawataninii . . . watakuwa bila ya udhuru, kabla wito huu wa madhabahuni haujafanywa.

184 Bwana Mungu na asaidie. Sasa huku mmeviinamisha vichwa vyenu, mkiomba kwa kicho.

185 Mnaona, yupo mama anayeketi hapa mbele zangu. Ameweka mikono yake usoni mwake. Anaugua ugonjwa wa uti wa mgongo. Naye pia ana wasiwasi. Ana ugonjwa wa tumbo. Naye ameketi hapa mbele zangu sasa. Na huenda anajua, hatoki katika nchi hii. Ametoka kwenye mji uitwao Macon. Naam. Je! unaamini Mungu anaweza kuniambia wewe ni nani? Wewe ni Bi. Ayers. Kama hiyo ni kweli, inua mkono wako. Hatufahamiani. Hiyo ni kweli, sivyo? Sasa shida yako imekwisha. Yesu Kristo; uligusa vazi Lake. Amekuponya. Sasa amini tu.

186 Yupo mwanamume anayeketi huko nyuma ya jengo. Anatafuta ubatizo wa Roho Mtakatifu. Anataka kubatizwa na Roho. Anasimama hapa mbele yangu. Hatoki hapa, pia. Anatoka

Carolina, Charlotte. Jina lake ni Lepoe. Amini kwa moyo wako wote, na Mungu atakujaza na Roho Mtakatifu, ndugu ya—yangu, kama utaamini.

187 Hapa, kwenye mkono wangu wa kuume, huyu hapa m—mtu na mkewe wameketi papa hapa mbele yangu hapa. Ni mume na mke wakongwe, kwenye mkono wangu wa kuume. Bibi huyu anaugua ugonjwa wa utumbo mpana. Mumewe ana ugonjwa wa moyo. Hawatoki hapa. Wametoka Tennessee. Bw. na Bibi Thomas, kama mtaamini kwa moyo wenu wote, inueni mikono yenu nanyi mwaweza kuukubali uponyaji wenu. Yesu Kristo anawaponya. Hivyo ndivyo hasa alivyoahidi kufanya. Lakini sijapata kuwaona watu hao maishani mwangu.

Usahaulifu wa kiroho!

188 Yesu alisema, "Kazi nizifanyazo Mimi ninyi nanyi mtazifanya. Bado kitambo kidogo, na ulimwengu hautaniona tena; bali mtaniona, kwa kuwa Mimi," kiwakilishi nafsi, "nitakuwa pamoja nanyi, hata ndani yenu, hata ukamilifu wa dahari." "Yesu Kristo yeye yule jana, leo, na hata milele."

189 Sasa, kwa wanaume na wanawake humu ndani, mlio na kasoro fulani, ambao kamwe hamwezi kuona jinsi. . . Ninyi, mnataka kuamini, bali kamwe hamwezi kuingia humo, nanyi mngetaka kuombewa, mnataka kumkubali wakati mkiwa katika Uwepo Wake, mwaweza kuja na kusimama papa hapa karibu nami, mniache niwaombee na kuwawekea mikono. Kama mngekuja papa hapa sasa, ninyi mnaoteseka namna hiyo, kwa usahaulifu wa kiroho, na mngetaka kuombewa, mpate kufunguliwa kutoka kwa huo. Kama wewe si—si mwaminio, bali unataka kuombewa, njoo hapa na usimame. Mungu akubariki, mvulana. Mtu mwingine aje? Mungu akubariki, mama. Njoo. Mungu akubariki, msichana. Mtu mwingine aje? Njoo, simama papa hapa, sasa hivi.

190 Usahaulifu wa kiroho, sitaki kutaabishwa na huo. Mungu aepushe. Hebu ni—hebu nife mauti ya—ya chochote, bali kamwe nisife mauti hayo ya asiyeamini.

191 Njoo, mkubali sasa. Sivyo? Njoni kutoka, na mshuke mje kutoka kwenye roshani, enyi marafiki. Ni hatua chache tu kufikia hapa chini, na huenda ikamaanisha tofauti kati ya mauti na Uzima, kwenu.

192 Angalieni, siwezi kumfanya Kristo kutenda lolote. Haimbidi Kristo kutenda lolote ila jambo moja: Yeye hana budi kulitimiza Neno Lake. Hana budi kufanya hivyo apate kuwa Kristo, kuwa Mungu. Hana budi kulitimiza Neno Lake.

193 Sasa kumbukeni, kama huna hakika na ujuzi wako, mbona usishuke uje sasa. Kama wewe ni mfuasi tu wa dhehebu, kama wewe ni mjukuu wa Kipentekoste, Mungu hana wajukuu. Anao wana na binti, bali sio wajukuu wa kiume na wa kike.

Mnaona? Mungu hana hao. Ana wana na binti tu, nawe unajua sivyo ulivyo.

194 Huenda umenena kwa lugha, huenda umecheza dansi, huenda umefanya yote *haya*. Hilo ni sawa. Sina neno dhidi yake. Lakini hata hivyo kama ungali una usahaulifu huo wa kiroho, shuka uje, na uje hapa na kusimama hapa. Hebu tuliombee. Wasemaje? Ewe mfuasi wa kanisa, mfuasi tu wa—wa kawaida wa kanisa, mbona usije hapa juu na tuliondolee mbali sasa hivi.

195 Sitaki kuondoka Birmingham hapa, na kujua ya kwamba siku moja, wakati Hukumu itakapokuja, nami sina budi kusimama mbele yenu . . . Kumbukeni, nitakutana nanyi tena. Kama sitakutana nanyi hapa kwenye hii, ama nitakutana nanyi kwenye ile Hukumu nami sina budi kuwajibika kwa yale niliyosema usiku wa leo.

196 Sasa sikilizeni. Tubuni, enyi marafiki! Tubuni, ondokeni kwake. Ondokeni humo. Njoni sasa.

197 Hilo linapaswa kumfanya kila mwanamke aliyekata nywele zake humu nchini, ama mahali hapa, kupanda hapa juu sasa. Hiyo ni kweli kabisa. Hiyo, kwamba huna neema ya kutosha kusema kweli, "Na—na—na—nataka, nataka kuziacha nywele zangu zikue, Ndugu Branham." Inapaswa . . . "Inanibidi . . . Vema, sina neema ya kufanya hivyo."

Mbona, unasema, "Hiyo ina uhusiano wowote nayo?"

198 Hapa si muda mrefu uliopita, mhudumu mashuhuri sana alinijia, akasema, "Ninataka kukuwekea mikono, Ndugu Branham." Kasema, "Kila mtu anakuchukua kama nabii."

Nikasema, "Kamwe sikusema nilikuwa nabii."

199 Akasema, "Lakini watu wanakuchukua hivyo. Daima unawakemea sana hao wanawake, kuhusu kuvaa kaptura," na—na, loo, Mpentekoste. Kisha kasema, "Kuhusu kuvaa kaptura, na kukata nywele zao, na kadhalika." Kasema, "Hiyo si kazi yako."

Nikasema, "Ni kazi ya nani basi?"

200 Naye akasema, "Hao watu, kwa nini usiwafundishe hao wanawake jinsi ya kuwa, kuwa na karama kuu za kiroho, na kuwasaidia watu, badala ya kujaribu kuninii . . . " Kasema, "Wanakuchukua. Yale uwaambiayo, wangekuamini." Kasema, "Kwa nini usiwaambie jinsi ya kupata karama kuu na kuwasaidia watu, badala ya sikuzote kuwahukumu?"

201 Nikasema, "Ninawezaje kuwafundisha aljebra wakati hawatajifunza ABC zao?" Mnaona? Mnaona?

202 Inakupasa kuanzia kutoka chini, tubu la sivyo utaangamia! Sasa unaweza kuchagua mwenyewe, tubu au uangamie! Yesu Kristo amejitambulisha kabisa hapa, usiku baada ya usiku. Na huu ndio usiku tuliokuwa tumeutenga kwa ajili ya wokovu huu.

Ni hatua chache tu kuja hapa, nami nina wakati mwingi sana wa kungojea.

203 Kumbukeni, Birmingham, damu yenu haiko juu yangu. Sina hatia. Na kama kweli una Roho Mtakatifu, una nafasi ya kuja sasa. Na kama unaugua namna fulani ya ukanisa ambao umekufanya kushikwa na usahaulifu wa kiroho, kwa nini usije? Yesu ndiye tiba. Mbona usije?

204 Sasa watu wengine waliondoka kwenye roshani. Nilikuwa nikingojea kuona mahali walipokuwa, wakitoka nje ama kuja madhabahuni. Hawa walio hapa chini, njoni huku. Hiyo ni kweli. Ninyi mlio hapa, njoni msimame karibu na madhahabu, useme, "Nimemalizana na hii." Naam, walikuwa wakishuka kuja, mama wawili. Hiyo ni sawa.

205 Njoni moja kwa moja huku juu sasa. Hatua chache tu kutoka kwake. Nazo hatua hizo huenda zikamaanisha tofauti yake.

206 Sasa, angalieni, ninataka kuwaulizeni jambo fulani. Vipi kama Yeye akija usiku wa leo? "Loo," mwasema, "Haji." Sijui kama anakuja au la. Hii ndiyo ishara ya mwisho. Kumbukeni, BWANA ASEMA HIVI! Mlipata kunisikia nikisema hivyo ila yaliyo kweli? Mnaiona ishara yenu ya mwisho. Hilo ni la Kimaandiko. Mmeiona ishara yenu ya mwisho, enyi Pentekoste. Msichanganyikiwe na yale aliyowaambia Israeli baada ya Kunyakuliwa; hiyo si ninyi. Mmekwisha, wakati huo. Mnaona? Sasa ni siku yenu. Sasa ni ishara yenu. Sasa ni wakati wenu. Msiukatae. Msifanye hivyo. Afadhali mje. Mnaamini mimi ni mtumishi wa Mungu? Kumbukeni.

207 Birmingham, sijapata kukutana na watu wazuri zaidi. Ninyi ndio watu wazuri kuliko wote ningalitaka kukutana nao maishani mwangu, bali mnahitaji uamsho. Mnakufa. Mnaambukizwa na usahaulifu wa kiroho. Mnakufa. Msifanye hivyo. Huisheni kile mlicho nacho. Kileteni tena, upesi, kabla Yesu hajaja.

208 Vema, wakati wakininii...Endeleeni kuja. Acheni waendelee kuja mpaka tutakapowapata wote, ambao Bwana anawaita, hapa juu. Njoni sasa.

209 Ondoeni usahaulifu huo. Tabibu mkuu yupo hapa sasa kuuponya huo, kuwaondolea. Amethibitisha ya kwamba Yeye yupo hapa. Ni wangapi watakaotambulisha hilo, kwa kuinua mkono wako, useme, "Kweli ninaamini; kwamba Yeye alisema angefanya hivi"? Mnaona? Sasa Yupo hapa. Mnaona? Mnaona? Aminini.

210 Basi ni wangapi wanaojua ya kwamba ninawaambia kweli, kwamba mnakufa na mnahitaji uamsho? [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.] Mnaona? Ni kweli.

211 Ninyi ni watu wazuri. Huwezi kupata wazuri zaidi. Hakuna mioyo bora inayopiga, kuliko chini ya maskini mashati haya ya

Kusini huku chini. Hiyo ni kweli, watu halisi! Lakini, jamani, afadhali muamke, upesi sana! [Ndugu Branham anapigapiga mimbarani—Mh.] Katika saa msiyodhania, huenda likatukia. Huenda lisitukie; sijui mimi.

212 Lakini, kumbukeni, mnapata onyo lenu la mwisho, kwa hiyo torokeni wakati mkiwa na wakati wa kutoroka. Njoni sasa. Mradi tu wanakuja, nitaendelea kungojea, kwa kuwa huenda kukawa . . . Nafsi moja ina thamani ya ulimwengu elfu kumi. Na mradi tu watu wanashawishika . . .

213 Ningetaka kuona huu ukianzisha uamsho mkubwa mno ambao utaliwasha kila kanisa huku; kama mngetupilia mbali tofauti zenu na mwondoe ubinafsi huo wote, na kumkubali Roho Mtakatifu. Mlidai mnaliamini. Mlidai kuliamini, na, inapofikia kujitambulisha Lenyewe, ndipo mtatengana. Mbona tusiiunganishe mioyo yetu pamoja na Neno la Mungu na kuiamini ile Kweli? Hivyo ndivyo. Mtaendelea tu kufa, kufa, nanyi mnaelekea moja kwa moja kwenye Laodikia. Jinsi hasa alivyoahidi, itakuwa hivyo. Hamtakuja sasa? Siku ndiyo hii. Huu ndio wakati uliokubalika. Angalieni yale Roho Mtakatifu atakayofanya.

214 Sasa ninawataka wahudumu wote hapa, wanaowajali watu hawa, waje waombe pamoja nami, pia. Njoni hapa juu, wahudumu wote wanaowajali watu hawa. Njoni, njoni tu papa hapa karibu, na mchangamane na watu, mhudumu ama mfanya kazi mahususi, mfanya kazi mzuri mahususi, mwanamke ambaye angetaka kusimama pamoja na wanawake hawa sasa. Nitaamini, kwa moyo wangu wote, ya kwamba Roho Mtakatifu ataingia mahali papa hapa sasa na kujitambulisha tu Mwenyewe miongoni mwa watu hawa wote.

215 Sasa hebu niwashauri watu hawa hapa, kwanza. Sasa, enyi marafiki, chochote kilichowaleta hapa, Yeye anajua. Nami ninaweza kuwathibitishia, itakuchukua, mmoja mmoja, kuwaleta hapa jukwaani, wala hapatakuwapo na jambo moja ambalo hatawajulisha. Sasa hiyo imekuwa tangu nilipokuwa mvulana mdogo. Karama hiyo haina tashwishi. Ila swali ni kwamba, je! mnaweza kuipokea? Mnaiamini? Sasa Yeye yupo hapa. Vema, kama Yupo hapa, basi kuna jambo moja tu, Yeye hulitimiza Neno Lake. Basi amini tu kwamba unalipokea, na kulikubali, na kusimama na kusema, "Bwana Mungu, nipo hapa kulikubali," na ukae tu pale mpaka litukie.

216 Kama vile Buddy Robinson alivyosema wakati mmoja, kwenye shamba la mahindi. Alisema, "Bwana, usiponipa Roho Mtakatifu, utakaporudi utakuta lundo la mifupa limewekwa hapa." Alilimaanisha kabisa. Nawe hutapata chochote kutoka kwa Mungu mpaka utakapodhikika vya kutosha.

217 Sasa, je! umewaona watu wa siku hizi, umeona kile tunachofanya siku hizi? Sisi, kwa kweli, tuna Mungu wa kutosha

kabisa hata tunapokuja jukwaani, tunasema, "Naam, labda afadhali nije huku." Sasa huu ndio ujuzi wa ulimwenguni kote. "Naam, afadhali niende kule na kusimama." Kasema, "Vema, vema, sijui. Mimi huyu hapa, mnaona." A-ha! Ni mahali pa jinsi gani kuwapo! Hakuna moto unaowaka. Hakuna hamu. Hakuna "liendee!" Na, kama mwinjilisti, hilo huniua tu kuwaona watu wa Mungu katika hali kama hiyo. Tunapaswa kuwa na moto.

218 Lakini, unaona, ni kitu gani? Ni vile hasa nilivyowaambia. Ufunuo 3, "Wewe ni vuguvugu. Na," Yeye akasema, "kwa kuwa wewe ni vuguvugu, basi nitakutapika kutoka kinywani Mwangu." Hiyo ni kweli? [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.] Hivyo ndivyo alivyosema. Na, kama alisema hivyo, hivyo ndivyo atakavyofanya. Kwa hiyo na tusiwe umati huo.

219 Wewe upo hapa, mhitaji. Hebu tulipate, ama tufe, papa hapa. Hiyo ni kweli. Hebu na tulipate, la sivyo tufe.

220 Sasa, ndugu yangu mpendwa, dada, kama ningeweza kushuka kuja huko na kukusaidia kufanya jambo fulani, hakika ningefanya hivyo. Sasa, kwa karama, ninaweza kukwambia kilichokuleta hapa. Ninaweza kukwambia ni kitu gani, kwa Roho Mtakatifu, kwa Roho wa Mungu, nikwambie kile kilichokuleta, kile umefanya, kile kitakachokuwa siku za usoni, ama kitu kama hicho; bali hilo halitoshi. Huna budi kulikubali Hili, wewe mwenyewe. Inapaswa kuwa ni wewe!

221 Sasa uko tayari? Inua mkono wako, useme, "Niko tayari. Niko tayari kufia papa hapa." Sasa usifanye hivyo isipokuwa unalimaanisha. "Niko tayari kufia papa hapa, ama nipate kile ninachotaka kutoka kwa Mungu." Amina. Mko tayari kweli? [Kusanyiko linashangilia na kusema, "Amina."—Mh.]

222 Basi hebu wasikilizaji wasimame, kila mahali. Sasa pamoja, pamoja, hebu tuungane pamoja. Na tuombe. Na hebu tuninii tu. . . Ninyi wahudumu sasa njoni kwa watu hawa hapa, kila mmoja, nanyi mnaiwakilisha mikono ya Kristo sasa.

223 Ninyi mnaotaka Roho Mtakatifu, ninyi mnaotaka tukio hilo, sio msisimko wa mhemko; mnataka Roho Mtakatifu, ule Uhai, chembe ya Uhai ndani yako. Nawe unataka kuuondoa huo usahaulifu unaokufanya hu—huwezi kujitambua; hujui unakosimama; hujui wewe ni nini; hebu tuuondoe sasa hivi! Kuna Kuzaliwa upya hapa kwa ajili yako, Kuzaliwa kupya halisi, kwa kweli.

224 Sasa hebu tuweke mikono yetu juu ya watu hawa. Hebu, kila mmoja, tuinue mikono yetu na kuomba kwa moyo mmoja.

225 Baba wa Mbinguni, katika Jina la Bwana Yesu, tujalie, Bwana, kwamba katika Jina la Yesu Kristo, kwamba Roho Mtakatifu atakuja usiku wa leo, Jumamosi hii usiku, ambapo Roho Mtakatifu alishuka kama upepo wenye nguvu ukienda kasi. Jalia watu hawa wabatizwe katika Roho Mtakatifu.

Jalia Moto na Nguvu za Mungu zisiwaache. Kama watakuwa hapa asubuhi, jalia wakae, wakae mpaka Roho Mtakatifu atakapokuja.

226 Wazo ndilo hilo! Hilo ndilo! Huyo hapo. Huyo ni Roho Mtakatifu akija.

[Ndugu Branham anazungumza na mtu fulani wakati akiondoka mimbarani—Mh.] Nilifanya hivyo. Najua hivyo.

Hivyo tu. Aminini sasa! Mkubalini! Jazweni na baraka Zake. [Kusanyiko linaendelea kuomba na kushangilia.]

Usahaulifu Wa Kiroho SWA64-0411
(Spiritual Amnesia)

Ujumbe huu uliohubiriwa na Ndugu William Marrion Branham, ulihubiriwa hapo awali katika Kiingereza mnamo Jumamosi jioni, tarehe 11 Aprili, 1964, kwenye National Guard Armory huko Birmingham, Alabama, Marekani. Kila jitihada imefanywa kuuhamisha ujumbe huu wa sauti kutoka kwenye kanda ya sumaku iliyorekodiwa na kuchapishwa bila kufupishwa katika Kiingereza. Tafsiri hii ya Kiswahili ilichapishwa na kusambazwa na Voice Of God Recordings.

SWAHILI

©2018 VGR, ALL RIGHTS RESERVED

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. BOX 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org

Ilani ya haki ya kunakili

Haki zote zimehifadhiwa. Kitabu hiki kinaweza kuchapishwa kwa matbaa ya nyumbani kwa matumizi ya kibinafsi ama kusambaza, bila malipo, kama chombo cha kuitangazia Injili ya Yesu Kristo. Kitabu hiki hakiwezi kikauzwa, kunakiliwa kwa wingi, kuwekwa kwenye mtandao, kuhifadhiwa kikatolewe tena, kufasiriwa katika lugha zingine ama kutumiwa kuomba fedha bila idhini halisi iliyoandikwa moja kwa moja kutoka Voice Of God Recordings®.

Kwa habari zaidi ama kwa vifaa zaidi, tafadhali wasiliana na:

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. BOX 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org